**RIPOTI MAALUM-2:** Ndoto ya Mwl. Nyerere yazimwa...

UKURASA 4

**WALIOVAMIA** eneo NSSF kuanza kuondolewa leo...

UKURASA 7



**ZUMA** akubali kuungana na Ramaphosa kuunda serikali...

UKURASA 19



**MBAPPE HATACHEZA OLIMPIKI**

UKURASA 22

Nipashe

Jumanne Juni 18, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581711

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardiannewspaper

LIKE & FOLLOW US

## EID MUBARAK

# Salamu zatawala uchaguzi, amani

UKURASA 2



Waumini wa dini ya Kiislam mjini Iringa wakiswali Swala ya Eid Al Adha katika Uwanja wa Samora jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# SMZ, Saudi Arabia kushirikiana uendeshaji wa shughuli za Hijja

UKURASA 17

**MAZIKO YA CHILIMA**

## Wanne wafariki dunia akiwamo mjamzito

UKURASA 19

**MICHEZO** **SIMBA YAFUATA BEKI KISIKI ASEC** UK 24

**MAONI, KATUNI UK.6**

EID MUBARAK

# Salamu zatawala uchaguzi, amani

Na Jenifer Gilla

WATANZANIA wamesisitizwa kuitumia haki yao ya kupiga kura katika uchaguzi wa serikali ya mitaa, vijiji na vitongoji utakaofanyika Novemba, mwaka huu na kuitumia mitandao ya kijamii kwa mambo yenye manufaa kwao na taifa.

Hayo yalisemwa jana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa katika swala ya Eid EL-Adh'haa iliyofanyika kitaifa katika Msikiti wa Mfalme Mohamed VI, jijini Dar es Salaam.

Alisema Mtanzania yeyote mwenye sifa ana haki ya kuchaguliwa ama kuchagua kiongozi anayeona kuwa anamfaa na ni wajibu wake kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji utakaofanyika Novemba, mwaka huu.

Waziri Mkuu aliwakumbusha pia kuhakiki majina yao katika daftari la mpigakura ifikapo Agosti, mwaka huu, ili wakati utakapofika watekeleze haki yao msingi ya kuchagua viongozi wanayemtaka.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, waliofikisha umri wa kupiga kura na waliohama maeneo, kwenda kujiandikisha kwenye daftari hilo katika maeneo yao ya sasa.

"Nikukumbushe tu kwamba unayo haki ya kuchaguliwa kuwa kiongozi, unayo haki ya kumchagua kiongozi unayempenda ambaye unaamini atakuletea maendeleo katika eneo lako," alisema.

Alisisitiza jamii kuitumia mitandao ya kijamii vizuri kwa kufanya mawasiliano yaliyo mema na mambo yenye manufaa kwa jamii badala ya kwenda kinyume na maadili ya nchi.

Alisema mitandao hiyo imeletwa kwa lengo jema la kuleta maendeleo ya mtu mmoja mmoja na taifa kama ikitumiwa vizuri na kwamba jamii inapaswa iyachuje kwa kuwa kuna mabaya yanayoharibu misingi ya taifa hilo.

"Umeletewa mtandao utumie vizuri, kwa mawasiliano yaliyo mema, usiutumie vibaya kwa kuwatukana watu, usiutumie kwa kutuma picha ambazo hazina maudhui mema," aliongeza.

Alisisita haja ya kuimarisha taasisi za malezi ya vijana ili kudhibiti mmomonyoko wa maadili na misingi ya kitanzania inayotokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa kuwa kundi hilo limeipokea vibaya.

Aliwakumbusha viongozi wa dini kutumia karama walizopewa na Mungu kuiongoza vizuri jamii ili kuwa na jamii inayozingatia misingi ya maadili na utamaduni wa nchi hiyo.

Waziri Mkuu pia aliliagiza Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) kusimamia weledi kwa taasisi zote zinazopeleka waumini wa dini ya Kiislam Makka, Saudi Arabia kwenye Hijja ili wasipate changamoto wanapokwenda na wanaporudi.

Aliwasihi waumini wa dini hiyo kujenga tabia ya upendo na kusaidiana kwa kuwajali na kuwakumbuka wasio na uwezo kama sikukuu hiyo inavyoelekeza kuwa wanapochinja wawakumbuke na wasiojiweza.

Aliwasisitiza pia kuachana na matumizi ya kuni na mkaa katika kupikia na badala yake watumie nishati safi ikiwamo gesi, umeme, na mkaa mbadala ili kutunza mazingira kwa kutokata miti na kuharibu vyanzo vya maji.

Alisema serikali inaendelea kutoa maelekezo ya ukomo kupikia kwa kutumia kuni na mkaa kwa taasisi zote zinazopika chakula kwa watu zaidi ya 20 ikiwamo shule, vyuo vikuu, magereza na makambi ya polisi na mabadiliko yameshaanza kuonekana.

Waziri Mkuu alisema lengo la serikali ni mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu, kupunguza matumizi ya nishati isiyo salama kupikia kwa asilimia 50 na mpaka kufikia mwaka 2030 wawe wamepunguza kwa asilimia 80.

Aliwakumbusha pia kushiriki kutoa maoni yatakayoboresha Dira ya Maendeleo wa Taifa ya mwaka 2026 hadi 2050 inayotarajiwa kuandaliwa na serikali.

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan jana aliungana na waumini wenzake katika Msikiti wa Mikocheni kwa Warioba, kwa swala ya Eid EL-Adh'haa.

Katibu Mkuu wa BAKWATA, Alhaj Nuru Mruma, aliwakumbusha Waislamu na Watanzania wote kuendelea kuwa kitu kimoja bila kujali misingi ya dini zao, kabila na itikadi za kisiasa ili kuienzi na kudumisha amani ya nchi hiyo.

Pia, aliwakumbusha Watanzania kushiriki haki yao ya kikatiba ya uchaguzi kwa kuomba kuchaguliwa au kuchagua viongozi wanaowapenda pamoja na kutunza mazingira kwa kupanda miti.



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na baadhi ya wananchi na waumini wa dini ya Kiislam baada ya kumalizika kwa Swala ya Eid Al Adha katika Msikiti wa Mikocheni kwa Warioba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

"Wito wetu kwa Waislamu wanaoona wanazo sifa za kuongoza wasiache fursa hii adhimu iwapite kwani ni haki yao ya msingi kikatiba inayotekelezwa kupitia vyama vyao vya siasa," alisema.

Aidha, aliziomba mamlaka zinazohusika na mchakato wa uchaguzi kuufanya kwa uwazi na weledi wakizingatia utoaji wa haki kwa kila anayestahiki ili wapatikane viongozi waliochaguliwa na wananchi na ambao wako tayari kuwatumikia kwa uadilifu.

Kaimu Mufti, Sheikh Ali Ngeruko, aliwakumbusha Watanzania kuacha vitendo vya ukatili kwa watoto kwa kuwanajisi na kuwaua kwa kuamini imani za kishirikina zinazowaelekeza kuwa wakifanya hivyo watakuwa matajiri.

Alisema hali hiyo imewafanya watoto kuwa waathirika wa masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa hali inayoweka maisha yao katika hatari na kutoijua hatima yao.

Alisema matukio hayo yanasababishwa na mmomonyoko wa maadili na changamoto ya afya ya akili na kuzisihi familia kuyatafakari matatizo hayo kwa umakini na kuwashirikisha wataalamu wa afya ya akili.

**KUWAKUMBUKA WAHITAJI**

Katibu wa Sekretarieti ya Baraza la Ulamaa Taifa (BAKWATA), Shekhe Suwed Twaibu, alisema waumini wa dini ya kiislamu wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kulinda amani wakati huu taifa linaingia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu 2025.

Shekhe Twaibu, alisema hayo jana wakati akitoa hotuba yake kwenye ibada ya Eid iliyofanyika katika viwanja vya Jamhuri jijini Dodoma.

"Mwaka huu itatupasa Waislamu kulinda amani yetu kwa kuwaepuka watu wanaopandikiza chuki, ili kuharibu amani yetu lakini pia tunao wajibu na haki ya kupiga kura kwa ajili ya kuchagua viongozi wetu lakini pia haki ya kugombea katika nafasi mbalimbli za uongozi tusibaki kuwa wasandiizaji," alisisitiza Shekhe Twaibu.

Naye Shekhe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, aliwataka waumini wenye uwezo kuwakumbuka watu wasio na uwezo wakiwamo wajane, yatima, wazee na watoto wanaolelewa kwenye vituo wanapoisherehekea sikukuu ya Eid.

Alitoa wito huo kupitia nasaha zake kwa waumini wa dini hiyo kwenye ibada iliyofanyika katika Msikiti Mkuu wa Gadaff, Dodoma.

Alisema kwenye sikukuu mara nyingi watu wasiojiweza wamekuwa wakisahaulika na watu wenye uwezo na kuomba jamii iwakumbuke ili na wao waweze kusherehekea kama ilivyo kwa wengine ambao wana nafasi ya kufurahia.

Aliwataka pia waumini wanapoisherehekea sikukuu hiyo kukumbuka kuiombea nchi, serikali na Rais ili taifa liendelea kuishi kwa amani na utulivu ukizingatia kuwa kuna nchi ambazo siku kama hiyo wako kwenye mapigano ya vita.

Kadhalika, waumini hao wamekumbushwa kuomba kwa ajili ya uchaguzi unaokuja ikiwamo wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu na uchaguzi mkuu mwaka 2025 kwa ajili ya kuchagua Rais, wabunge na madiwani.

Hata hivyo, aliwataka waumini wa dini ya kiislamu kuendeleza umoja na mshikamano uliopo pamoja na kuwa na moyo wa kuombeana, kupendana na kuulinda uislamu wao kama walivyoagizwa na Mtume wao.

**Imeandikwa Jenipher Gilla (DAR), Paul Mabeja na Peter Mkwavila, (DODOMA)**

## HABARI KITAIFA

# Mpango: Chilima atakumbukwa uongozi imara

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema Makamu wa Rais wa Malawi, Hayati Dk. Saulos Chilima, alikuwa kiongozi imara, mwanajumuiya wa kweli wa Afrika ambaye wakati wote alitanguliza mbele maslahi ya wananchi anaowangoza na Afrika.

Akizungumza jana wakati ya ibada ya mazishi ya kiongozi huyo katika Uwanja wa Taifa wa Bingu, Lilongwe nchini Malawi, ambako akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kiongozi huyo atakumbukwa kwa mengi aliyoyafanya kwa wananchi.

Makamu wa Rais alimtaja Hayati Chilima kama kiongozi aliyesimamia umoja, amani na usalama, mageuzi ya kiuchumi ya Malawi na utawala wa kidemokrasia nchini humo.

Alisema Tanzania inatoa salamu za pole na kuungana na waombolezaji wote walioguswa na msiba huo katika kipindi hiki kigumu.

Alisema wananchi wa Malawi na ukanda wote kwa ujumla wanapaswa kumuenzi Hayati Chilima kwa kuendeleza yale aliyosimamia na kuendelea kumwombea apumzike kwa amani.

Katika kushiriki mazishi hayo ya Kitaifa, Makamu wa Rais ameambatana na Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hamza Hassan Juma, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stephen Byabato pamoja na Balozi wa Tanzania, Agnes Kayola.




N THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.12179 OF 2024
In the Matter of the Estate of the late
SELESTINI BERNARD MNYANDWA

By 1.BERNARD ALOYCE CHIBINDA
2..........................................

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 27th day of JUNE 2024.
Dated at Morogoro this 10 day of JUNE 2024.

................................
RESIDENT MAGISTRATE

KUPOTEA KWA CHETI



**DONARD BARNABA KIULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha Darasa la Saba chenye index namba PS 1801082-003 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia ULEMO PRIMARY SCHOOL mwaka 2017. Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA KIO/378/2024**

KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**GELENYA WAPI KUBILU**
anatangaza kupotelewa na Nyaraka ya umiliki wa Kiwanja Namba 24 Kitalu "45" kilichopo Kizumbi Manispaa ya Shinyanga Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi Kilichopo karibu.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/SHI/SHI/4443/2024**

KUPOTEA KWA CHETI



**MWANAHERI HABIBU MSONDE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0739-0107 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia HIJRA SEMINARY SECONDARY SCHOOL mwaka 2006. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/MAN/KIT/221/2024**

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.12635 OF 2024
In the Matter of the Estate of the late
IRIOKO ELIUDI KITURURU

By 1.YULIA IRIOKO KITURURU
2..........................................
ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 20th day of JUNE 2024.
Dated at Morogoro this 04th day of JUNE 2024.

................................
RESIDENT MAGISTRATE

## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha **Nipashe** au **The Guardian** kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

RIPOTI MAALUM -2

# Viwanda vya Nyerere vinavyogeuzwa maghala ya bidhaa kutoka nje ya nchi

**Na Mwandishi Wetu**

**HII ni sehemu ya pili ya ripoti inayoangazia kiwanda cha UFI (Ubungo Farm Implements) cha Shekilango, mkoani Dar es Salaam, ambacho badala ya kuzalisha zana za kilimo kama ilivyokuwa dhamira ya mwasisi wake, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, hivi sasa kinazalisha mabomba ya maji.**

**Katika sehemu ya pili jana, kulikuwa na ufafanuzi wa kina namna kiwanda hicho kilivyokuwa tegemeo nchini kwa uzalishaji zana za kilimo, kikihakikishia wananchi upatikanaji zana hizo nchini kwa bei nafuu. Endelea...**

UFI ni miongoni mwa viwanda vilivyojengwa na serikali chini ya serikali ya awamu ya kwanza, lakini hivi sasa vimegeuzwa maghala ya bidhaa mbalimbali kutoka China kama inavyoshuhudiwa kwa viwanda vya nguo vya Urafiki mkoani Dar es Salaam na Mbeya Textile mkoani Mbeya.

Hivi karibuni, mtandao wa Jamii Forums ulichapisha orodha ya mashirika na viwanda 32 ambavyo vimegeuzwa maghala ya bidhaa mbalimbali kutoka nje ya nchi huku nyumba za wafanyakazi wa viwanda hivyo zikitumika kama ofisi na maghala.

Orodha hiyo inajumuisha mashirika na viwanda ambavyo baada ya kubinafsishwa, ama vimekufa au kubadilishwa matumizi. Hivyo ni pamoja na Kampuni ya Bia Tanzania (Dar & Arusha Plants) 1993, TBL Farms Limited 1993, TBL Farms Ltd 1993, Tanzania Malyings Limited 1993, Mwanza Breweries 1993, Mwanza Tanneries 1993, Shamba la Mkonge Mosowero (TSA) 1992, Shamba la Mkonge Rudewa (TSA) 1992, Shamba la Mkonge Toronto TSA (1993), Shamba la Mkonge Mnazi (TSA) 1993, Shamba la Mkonge Mkumbara (TSA) 1993 na Shamba la Mkonge Ndungu (TSA) 1993.

Mengine ni Tanzania Tanneries-Moshi 1993, Morogoro Tanneries 1993, TANELEC 1995, News Africa Hotel 1993, ALAF ambayo iliuzwa 1995, Morogoro Shoes 1993, Morogoro Canvas 1994 na Tanga Cement Company 1995.

Orodha hiyo pia ina: Imara Wood Products Company 1993, Buckreef Gold Mining C 1993, Williamson Diamonds 1994, New Almasi Company 1994, MOPROCO 1995, Pugu Kaolim Mines Ltd 1993, Tanzania Cigarettes Company 1995, Lupa Gold Mines 1994, Light Source Manufactures 1994, Urafiki 1996, State Travel Services 1996 na NABICO 1996.




Akiwa Mburahati, Dar es Salaam wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu 2020, Rais John Magufuli, alisema kiwanda cha UFI kilijengwa kwa lengo la kufikia azima ya nchi ya viwanda, akiahidi kukifufua ili zana za kilimo zipatikane nchini.

Rais Magufuli alisema ufufuaji kiwanda hicho na vingine vilivyoanzishwa na Mwalimu Nyerere ndio sababu ya kutekeleza Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) litakalozalisha MW 2,115 (sasa linazalisha MW 470).

Kukiwa na dhamira hiyo serikalini, mwaka 2020 Shirika la Habari la China (Xinhua News) lilitangaza Tanzania imepata mkopo wa Dola za Marekani milioni 110 (Sh. bilioni 285.871) kujenga kiwanda cha kutengeneza matrekta kiitwacho URSUS_TAMCO cha mkoani Pwani. Kilianza kuunganisha matrekta mwaka 2017.

Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Adelhem Meru, alinukuliwa akisema, "Tumepata mkopo kutoka Poland ambao tutautumia kujenga kiwanda cha kutengeneza matrekta na zana nyingine za kilimo. Tanzania itakuwa nchi ya kwanza katika eneo la Kusini mwa Jangwa la Sahara kufungua kiwanda cha kutengeneza zana za kilimo."

Mwandishi alipohitaji kupata maoni ya Khamis Mgonda juu ya uamuzi huo wa serikali, mwananchi huyo alisema: "Mkopo ni mzuri lakini mimi siafiki uamuzi wa kujenga huko Kibaha (Pwani). Kwanini tusikifufue kiwanda cha UFI ambacho kipo? Kinahitaji ukarabati tu na maboresho ya kisasa.

"Zamani UFI ilikuwa mkombozi kwa wananchi kupata pembejeo za kilimo. Maoni yangu ni kwamba tufufue kiwanda cha UFI tupunguze gharama za ujenzi wa majengo ya kiwanda kipya."

Mbunge wa Musoma Vijijini (CCM), Prof. Sospeter Muhongo, hayuko mbali na wanaonyooshea kidole kinachoendelea katika kiwanda cha UFI, akisitikishwa na taarifa za kutozalishwa tena zana za kilimo kiwandani huko.

Prof. Muhongo ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Nishati na Madini katika uongozi wa Rais Magufuli, anasema Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere alijenga kiwanda cha UFI kwa lengo la kuboresha uchumi na ustawi wa taifa.

"Baba wa Taifa alithamini kilimo na kuwekeza katika viwanda vya zana za kilimo kama UFI, kiwanda cha mbolea, viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na ufugaji, vyuo vya kuzalisha wataalamu wa kilimo wa ngazi mbalimbali na vyama vya ushirika.

"Pia alithamini ushirikiano na nchi za nje kwenye sekta ya kilimo, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) lenye mashamba ya kilimo pamoja na tuzo na sherehe za wakulima. Alipeleka vijana nje ya nchi kusomea masuala mbalimbali ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Inaumiza leo kuona kiwanda chake cha UFI hakizalishi tena zana za kilimo," anasema Prof. Muhongo.

Inaporejewa historia ya viwanda nchini, UFI ni kampuni iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Kampuni. Kilianzishwa kwa fikra na misingi ya siasa za ujamaa na kujitegemea katika harakati za kutimiza utoaji mahitaji muhimu ya wakulima.

Kiwanda cha UFI kilijengwa kwa msaada na ushirikiano wa Serikali ya Watu wa China. Shughuli za ujenzi na ufungaji mitambo zilikamilika na kukabidhiwa rasmi kwa serikali mwaka 1968, mwaka mmoja baada ya Azimio la Arusha ingawa kuanza kwake rasmi kunatajwa kuwa Machi 4, 1970.

Kiwanda kimebadilishwa matumizi wakati ambao Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anasema sekta ya kilimo inachangia asilimia 26 katika Pato la Taifa, inatoa ajira za moja kwa moja kwa asilimia 62 ya wananchi, inaingiza asilimia 4.5 ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nje (Dola bilioni 2.3 kwa mwaka) na kuchangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda nchini.

**Itaendelea kesho**


SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WAFANYAKAZI TANZANIA – TUCTA
CHUO CHA WAFANYAKAZI TANZANIA – MBEYA

## TANGAZO LA KAZI

**1.0 NAFASI YA KATIBU MUHUTASI (SECRETARY) DARAJA LA III NAFASI 1 KATIKA CHUO CHA WAFANYAKAZI MBEYA.**

**2.0 MAJUKUMU YAKE.**

- Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida, kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kupata huduma kwa haraka.
- Kusaidia kutunza taarifa / kumbukumbu za matukio, mihadi wageni, tarehe za vikao, safari za mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anayofanyia kazi na kutoa taarifa kwa mkuu wake kwa wakati.
- Kusaidia kutafuta na kumpatia mkuu wake Majalada, Nyaraka au chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi.
- Kusaidia kufikisha maelekezo ya mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa anazokuwa amepewa na wasaidizi.

**3.0 SIFA ZA MWOMBAJI**

- Mwombaji awe mtanzania aliyehitimu kidato cha nne (form iv) au cha sita (form vi)
- Awe amehudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu uhazili na kufaulu ngazi ya stashahada katika chuo kinachotambulika na serikali.
- Mwombaji awe amefaulu somo la hati mkato ya Kiswahili na kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe na ujuzi wa internet na barua pepe.
- Mwombaji awe mchapakazi, mwaminifu na mwenye uwezo wa kutumika katika Nyanja mbalimbali za taaluma yake.
- Umri wa mwombaji usizidi miaka 45

**4.0 VIAMBATANISHO.**

- Barua ya maombi ya kazi yenye picha ya hivi karibuni upande wa kushoto.
- Taarifa binafsi (wasifu/ cv)
- Nakala za vyeti vya taaluma na cheti cha kuzaliwa, vilivyothibitishwa na wakili au mwanasheria.

**5.0 MAOMBI HAYA YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO.**

**Mkuu wa chuo,**
**Chuo cha wafanyakazi Tanzania,**
**S.L.P 3454 mbeya au kwa barua pepe:labourtz@gmail.com, maombi yatumwe ndani ya siku saba (7) baada ya tangazo hili kutoka.**

# Vijana 1,000 wanufaika kuboresha mawazo kibiashara

**Na Denis Mambya,**
MOROGORO

MKURUGENZI Mtendaji wa Chemba ya Wafanyabiashara, Viwanda na Wakulima Mkoa wa Morogoro, Mona Mapunda, amesema mradi wa imarisha sekta binafsi umewafikia na kuwanufaisha vijana 1,000 nchini kuendeleza mawazo yao.

Akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Uandishi wa Habari Morogoro (MSJ), alisema kwa kutambua umuhimu wa vijana, mradi huo umelenga kuimarisha sekta binafsi ikiwa ni pamoja na kuwainua vijana kujikwamua kiuchumi.

Alisema mradi huo uliwanufaisha vijana hao kwa asilimia 75 huku asilimia 25 kupatiwa vifaa kazi pamoja na mkopo wa asilimia 100 mwishoni mwa mradi wa imarisha sekta binafsi kwa kuwa vijana wengi hushindwa kuyaendeleza mawazo yao katika nyanja mbalimbali ikiwamo biashara.

Andwele Mwambene, mlezi wa wanafunzi wa chuo hicho aliitaja semina hiyo kuwa ni fursa kwa vijana ikiwamo kuondokana na dhana ya kuajiriwa serikalini ama taasisi binafsi na kujikita katika ubunifu.

“Vijana wengi hushindwa kutambua fursa nyingi zilizoko mbele yao bali hii semina kutoka chemba ya wafanya biashara, viwanda na wakulima imewapatia vijana wetu elimu hii na ni imani yangu kuna kitu kipya kitazaliwa ndani ya vijana hawa,” alisema Mwambene.

Lucas Alex mwanafunzi wa ngazi ya stashahada, alisema semina hiyo imepanua akili kwa kuwa hapo awali hakuwaza kujiajiri, sasa ametambua umuhimu wa fursa mbalimbali hapa nchini.

Twisila Dickson mwanafunzi wa ngazi ya stashahada, alisema semina hiyo imempatia elimu na kumjenga katika maarifa ya kuzitumia fursa ikiwamo kuanzisha biashara kwa kuwa chemba ya wafanyabiashara, viwanda na wakulima ili mhakikishia kumsaidia katika ukuzaji wa wazo lake.

Kwa kutambua umuhimu wa vijana hapa nchini chemba ya wafanya biashara, viwanda na wakulima imerahisisha gharama nafuu ya uanachama ambayo ni Sh. 20,000 ili kuwapa fursa itakayo wawezesha vijana kupanaua mawazo, ambayo itawasaidia kujikwamua kiuchumi.

## Shule 10 zakabidhiwa mashine za kudurufu

**Na Jumbe Ismailly,**
MANYONI

SHULE za msingi na sekondari 10 katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida zimepokea msaada wa mashine za kudurufu mitihani na kuondokana na utaratibu wa kuwachangisha fedha wazazi na walezi.

Ofisa Elimu Kata ya Muhalala, Mashaka Ringi, alisema msaada huo utaleta mapinduzi makubwa katika taaluma kwenye shule hizo.

Kwa mujibu wa Ringi shule hizo zilikuwa na uhaba mkubwa wa mashine za kudurufu na nyingi zilikuwa zikitumia gharama kubwa kwa ajili ya kuzalisha mitihani yao au mazoezi ya mara kwa mara yanayotakiwa ili yaweze kukidhi viwango vya elimu.

“Tunaamini kwa kupitia msaada huu ama msaada huo ambao umetolewa na ndugu yetu Nyalandu tunaenda kufanya mabadiliko makubwa sana katika sekta ya elimu, hususani katika taaluma zetu,” alisisitiza Ringi ambaye pia ni Mkuu wa Shule ya Sekondari Muhalala.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kintinku, Mateso Bwire, alisema shule hiyo ilikuwa na changamoto nyingi kwa sababu ina idadi kubwa ya wanafunzi na wakati wa kipindi cha mitihani walikuwa wakitumia gharama kubwa kudurufu mitihani.

Aidha, alimshukuru mdau aliyetoa msaada huo na kwamba kupatikana kwa mashine hizo kutaendelea kutatua changamoto iliyokuwa ikizikabili shule zilizopo katika halmashauri ya wilaya hiyo.

“Kwa hiyo ninamshukuru kwa asilimia kubwa na pia tupende kusema kwamba kama wapo wengi wa moyo kama wa huyu bwana huyu mfadhili, basi waje wajitokeze kwa wingi kwa sababu ukiangalia shule zilizopewa ni shule chache, lakini Wilaya ya Manyoni ina shule nyingi,” alifafanua.

Akikabidhi msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 15, mdau wa maendeleo wa Wilaya ya Manyoni, Joseph Nyalandu, alisema unalenga kuwapunguzia wazazi na walezi wa wanafunzi gharama walizokuwa wakitumia wakati wa kudurufu mitihani.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jumanne Mlagaza, alisema kupatikana kwa chombo hicho kutaisaidia pia ofisi ya utawala kutoendelea kutoa nyaraka za serikali nje ya ofisi na kusababisha siri za serikali kuanikwa hadharani.

Shule zilizopokea msaada huo ni pamoja na sekondari za Makanda, Chikuyu, Makuru, Mkwese, Mhalala, Masemapya, Sanza na Heka, wakati kwa shule za msingi ni Kintinku na Lusilile.




KWA USALAMA WA TANZANIA IJAYO

Miaka 5 ya Benkibima (Bancassurance), Ujenzi wa Sekta Inayoshamiri na Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima Nchini

Sekta ya bima nchini inakua kwa kasi kubwa. Katika kuelezea mafanikio hayo Kampuni ya The Guardian Limited (TGL), itachapisha matoleo maalum katika magazeti yake ya **The Guardian** na **Nipashe** mwezi ujao yatakayojikita kuangalia upatikanaji huduma za bima zenye matokeo chanya kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Matoleo hayo yatajikita zaidi kuelezea:

- **Mafanikio ya Benkibima kwa Kipindi cha Miaka Mitano**
- **Jitihada za Kitaifa Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima**
- **Mwelekeo wa Sekta ya Bima katika Serikali ya Awamu ya Sita**

Mradi huu wa ujumuishi wa huduma za kifedha ni jukwaa linalotoa fursa ya kipekee kwa watoa huduma za bima na wadau wengine kuonesha jinsi wanavyochangia ongezeko la upatikanaji huduma za bima na mapokeo yake nchini.

Usikose kutumia nafasi hii adimu kunadi taasisi yako na suluhisho bunifu dhidi ya majanga.

**Ili kupata maelezo zaidi ya jinsi ya kushiriki:**
**Wasiliana nasi kwa simu: 0714 791747, 0763214317, 0753 01427**
**Barua Pepe: advertise@guardian.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhalifu mitandaoni ukemewe

**MAPAMBANO** dhidi ya uhalifu mitandaoni ni jambo muhimu hasa wakati dunia ikiwa kwenye mabadiliko ya kutumia teknolojia ya mawasiliano.

Kuna mambo mengi yanayotokea katika kipindi hiki huku wahalifu wakitafuta mbinu mbalimbali za kuhakikisha wanakwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Dunia kwenda na mabadiliko ya teknolojia ni kurahisisha kazi na kupunguza muda unaotumika kwa binadamu kuifanya kazi hiyo.

Hata hivyo, kuna watu wanaotumia fursa hiyo kujinufaisha na kuona hawaachwi nyuma kwa jambo lolote lile.

Miaka ya nyuma kabla ya teknolojia ya mawasiliano haijabadilika, kazi nyingi zilikuwa zikifanyika kwa kwenda sehemu husika, lakini sasa hivi mtu anaweza kukaa nyumbani na akamiliza kila kitu kwa kutumia simu yake ya mkononi.

Siku za nyuma sehemu zenye huduma muhimu kama ulipaji wa bili za umeme, maji na benki, mtu ilibidi aende kwenye ofisi hizo hali iliyokuwa ikisababisha msongamo mkubwa wa watu.

Sasa hivi hata ukiwa nje ya nchi unaweza kufanya miamala na kulipia bili zako kwa wakati.

Kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi ilikuwa inachukua muda kumtumia ndugu yake pesa, lakini kwa sasa teknolojia imerahisisha, hakuna usumbufu tena.

Lakini, teknolojia hiyo imeingiliwa na kutumika vibaya kwa baadhi ya wahalifu kwenye sekta ya fedha kwa kuwaibia watumiaji na kuwafanya waogope kuitumia.

Mamlaka ya Mawasiliano Nchini (TCRA), imeeleza wazi kuwa inaendeleza jitihada za kupambana na kudhibiti uhalifu mitandaoni, ikiwamo huduma za kifedha kutokana na kuongezeka mifumo mipya ya mawasiliano ya teknolojia.

Inapokuja teknolojia mpya ni muhimu ikatumika vizuri ili kunufaisha watu na kuondoa ugumu uliokuwapo mwanzo.

Kwa nchini Tanzania, wafanyabiashara, wajasiriamali wamerahisishiwa kazi kwa kutumia teknolojia ya mawasiliano ambapo kwa sasa wanaweza kutuma pesa nje ya nchi na kuletewa bidhaa wanazotaka badala ya kusafiri hali inayowapunguzia gharama.

Katika matumizi ya teknolojia hii pia kunahitajika uaminifu wa hali ya juu ndio maana hata TCRA ikiwa ni mdhibiti wa matumizi mabaya ya mawasiliano imekuwa ikiingilia kati kila inapoona mambo hayaendi sawa.

Kuna wanaotumia teknolojia hiyo pia kwa malengo mabaya ya kuwachafua watu wengine kwenye mitandao.

Viongozi wa juu wanapokuwa kwenye majukwaa wamekuwa wakikemea tabia hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa kama isipodhibitiwa itarudisha nyuma maendeleo.

Duniani mabadiliko ya kiteknolojia hayawezi kuepukika, hivyo ni muhimu wadhibiti wa uhalifu mitandaoni kuwa makini kudhibiti hali hiyo ili kuepuka matumizi mabaya.


Hali hiyo imekuwa ikishamiri kwenye mitandao ya kijamii kiasi cha kuharibu hali ya hewa na wengine wanaochafuliwa huathirika kisaikolojia.

Wengine hudiriki kutengeneza picha na kufanya ionekane kama ya mhusika waliyepania kumharibia. Kwa kweli matumizi haya ya teknolojia hayatumiki kama ilivyokusudia kwa walioanzisha kuleta mabadiliko yawe ya kihabari au kiuchumi.

Uhalifu huu unapaswa kupigwa vita na kila mtu awe mlinzi wa mwenzake kwa kutokubali kusambaza picha yoyote inayodhalilisha utu wa mtu mwingine, kuharibu sifa au kufanyika kwa wizi wa aina yoyote.

Watu wote wakisaidiana na TCRA, uhalifu wa kimtandao utapungua na wengine wenye kusudio hilo wataacha kufanya hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Tuntule Swebe

# Jali, moshi huu wa injini unaua

**SUMU** na taka za sumu zinazotoka kwenye injini si salama, zina karbon au hewa ukaa inayoweza kukuua, kuchafua hewa na chakula au bidhaa.

Ndiyo maana wataalamu wa afya wanasema kufanya kazi, kula vyakula vilivyochafuliwa au kukaa karibu na moshi ambao una gesi hizo kwa kiasi kikubwa ni hatari kwa yeyote.

Ikumbukwe kemikali na hewa hii hutoka wakati injini zinazotumia petroli au dizeli zinapopumua na moshi huo kusambaa angani na pembeni.

Huwafikia walioko pembeni mwa barabara na kusababisha kupata madhara yanayojificha lakini yanayoweza kuibuka baada ya miaka kadhaa.

Baada ya miaka mingi au muda mrefu magonjwa yanayotokana na hewa chafu huanza kuonekana, kuanzia machoni, kifuani, kwenye ngozi na kooni kote yakisababisha athari.

Kwa kawaida moshi huo huumiza macho, pua na koo na harufu yake inaweza kusababisha kichefuchefu lakini wengi huchukulia kuwa ni kitu cha muda mfupi.

Uchunguzi wa kiafya unaonyesha kwamba baadhi ya watu waliovuta moshi mzito wana matatizo kwenye mapafu yanayosababisha kupumua kwa shida, mafua, kukohoa mara kwa mara na kuwa na mzio au aleji.

Kuzoea kuvuta moshi huu kunaweza kusababisha athari za haraka kama kuwashwa machoni, puani na koo kuk-ereketwa na hata mafua.

Inaelezwa na wataalamu kuwa moshi wa injini za magari, pamoja na bajaji na pikipiki unaweza kuleta madhara makubwa kama kwa afya watu na mimea hasa iliyo kando ya barabara.

Lakini, inavyoelekea wengi hawalielewi tatizo hilo na wala hawachukui tahadhari, mfano wafanyabiashara za vyakula karibu na barabara wana hatarisha maisha yao na wateja wao pia.

Kwa mfano, wale wanaouza vyakula mfano pweza, kachori, mishkaki, chipsi na vitafunwa kwenye stendi za mabasi mijini au kwenye barabara vinachafuliwa na vumbi pamoja na moshi wa vyombo vya moto.

Ni vyema wajue kuwa hula na kuishi kwenye kemikali za simu inayotoka kwenye injini.

Wanaokula na wanaotayarisha huweza kuugua magonjwa kama kuharisha, kutapika, kuhara damu, tumbo kujaa gesi, kupata kichefuchefu na kukosa hamu ya kula.

Ni vyema kukawa na udhibiti wa biashara ikiwamo kuuza vyakula karibu na barabara au vituo vya mabasi ambako magari hupumua. Aidha hata kukataza kupanda mboga barabarani ambazo huchafuliwa na moshi wa injini.

Wafanyabiashara wa vyakula, matunda, wakulima wa mboga na matunda pembeni ya barabara na wauza mboga hizo pembezoni wajiepusha na hatari hizo za kiafya.

Jamii nayo inahitaji elimu na kupewa ufahamu kuhusu madhara ya kula vyakula vilivyochafuka na sumu hasa za kemikali za moshi wa injini ili kujiepusha na magonjwa.

Bila shaka wafanyabiashara, wakulima kila mmoja kwa pomoja wanatakiwa kuwa na tahadhari kwani magonjwa ni sababu ya kuyumba kwa maendeleo kwenye ngazi za familia, jamii na taifa pia.

Visingizio kuwa wanatafuta fedha za kujikimu ndiyo maana wanalima au kuuza bidhaa za vyakula zilizochafuliwa na moshi wa injini kisikubalike kwani vyote vinadhuru afya.

Ni vema kufikiri kuwa hata usipoathirika leo kwa kupata magonjwa yanayoambatana na moshi huo hapo baaadaye kuna hatari ya kusumbuliwa na maradhi kwani mtu anapokua na umri mkubwa matatizo ya kiafya yaliyojificha kwa muda mrefu huibuka.

Ikumbukwe kuwa ni bora kuchukua tahadhari kwani kadiri watu wanavyozeeka, mifumo ya kinga hudhoofika vilevile, uzee una uwezekano mkubwa wa kuwa na changamoto za kiafya kuliko ujana.

Ni muhimu kuwa na tahadhari na umakini kwa kuukwepa moshi wa petroli na dizeli na kuacha kufanya biashara karibu na barabara ili kujikinga na magonjwa ambayo yanaweza kuepukika hasa kutoka kwenye vyombo vya moto.

HABARI KITAIFA

## NIDA kutumika uboreshaji Daftari Kudumu Wapigakura

**Na Christina Mwakangale**

NAMBA ya Utambulisho wa Taifa (NIN), iliyoko katika kitambulisho kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ni miongoni mwa nyaraka muhimu wakati wa mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura.

Ingawa kitambulisho si hitaji la kikanuni, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imesema kwamba, Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN), itasaidia kurahisisha uboreshaji wa mifumo ya uandikishaji, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Daftari na TEHAMA wa INEC, Stanslaus Mwita, aliyasema hayo Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, wakati akiwasilisha mada kwa waandishi wa habari kuhusu Mfumo wa Uboreshaji Daftari la Wapigakura na vifaa vinavyotumika.

"Mwaka huu NIDA itatumika kurahisisha kuboresha daftari wa wapigakura na kuweka katika mfumo. Namba ya NIN si hitaji la mpigakura kuandikishwa, ila itatumika kusaidia kuboresha," alisema Mwita.

Akifafanua, alisema mfumo wa uandikishaji wa wapigakura (Voters Registration System-VRS), umefanyiwa usanifu na kuboreshwa, ili kukidhi aina ya BVR (Biometric Voter Registration (BVR kits), za kisasa zinazotumia programu endeshi ya Android.

"Tofauti na BVR kits za awali ambazo zilikuwa zinatumia programu endeshi ya Windows. Mpigakura anayerekebisha taarifa zake kwa njia ya mfumo huu (mpya), ni sharti awe na namba ya NIDA," alieleza Mwita.

Pia kutokana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, wapigakura 5,586,433 wapya wanatarajiwa kuandikishwa ambao ni sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 waliopo kwenye daftari baada ya uboreshaji wa mwaka 2019/2020.

Wapigakura 4,369,531 wanatarajiwa wataboresha taarifa zao, ingawa idadi inaweza kuongezeka kutokana na Watanzania ambao walikuwa na sifa za kuandikishwa kuwa wapigakura mwaka huo, hawakuweza kujiandikisha kwa sababu tofauti.

"Wapigakura 594,494 inatarajia wataondolewa kwenye daftari kwa kukosa sifa za kuendelea kuwapo kwenye daftari. Baada ya uboreshaji (mwaka huu), inatarajiwa daftari kuwa na wapigakura 34,746,638."

**"Tofauti na BVR kits za awali ambazo zilikuwa zinatumia programu endeshi ya Windows. Mpigakura anayerekebisha taarifa zake kwa njia ya mfumo huu (mpya), ni sharti awe na namba ya NIDA," alieleza Mwita.**



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda akizungumza na wakazi wa Mtaa wa Malela, Toangoma Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam kuhusu hatua zitakazoanza kuchukuliwa kwa waliovamia maeneo ya NSSF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliovamia eneo NSSF kuanza kuondolewa leo

**Na Mwandishi Wetu**

WALIOVAMIA ardhi ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kuanza kujenga makazi katika Mtaa wa Malela, Kata ya Toangoma, Temeke Dar es Salaam wataanza kuondolewa rasmi katika maeneo hayo kuanzia leo.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa aliyoyatoa Juni 5, mwaka huu, wakati alipofika eneo hilo na kuwakamata watuhumiwa wanne wanaodaiwa kuwatapeli wananchi kwa kuwauzia maeneo yanayomilikiwa kihalali na NSSF na kuagiza wavamizi wote wa ardhi kuondolewa.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Sixtus Mapunda, alifika eneo hilo Juni 15 na kuendelea kutia msisitizo NSSF itatekeleza maelekezo yake ya kuwaondoa waliovamia maeneo ya miundombinu ya barabara na maji.

Mapunda alisema eneo la Malela historia inaonesha kuwa kati ya mwaka 2000 na 2002 serikali ilichukua eneo hilo kupitia Wizara ya Ardhi na ikawalipa fidia wakazi wote wa asili na kuwa mwaka 2005 mpaka 2008 Wizara ya Ardhi ilikuwa inayagawa kwa kuyauza maeneo hayo kwa watu binafsi na mashirika ikiwamo NSSF ambayo iliuziwa eneo hilo na walipewa hatimiliki.

Alibainisha kuwa kati ya mwaka 2012 na 2017 kwa nyakati tofauti, wananchi walianza kuvamia eneo hilo na kuwa kati ya mwaka 2020 na 2022 uliitishwa mkutano wa wavamizi baina ya NSSF na uongozi wa serikali na katika kueleweshana ikaonekana si busara waliovamia kipindi hicho kuondolewa na wakakubaliana kuwa waliovamia waingizwe kwenye mpango wa matumizi ya ardhi na NSSF.

"Baada ya hapo yakawekwa makubaliano kuwa walioingizwa kwenye mpango na NSSF washirikiane na Mfuko wasiwepo watu wengine watakaovamia, lakini kilichotokea kati ya mwaka 2002, 2003 na 2004 waliovamia walikuwa wengi kuliko wale waliokuwapo mwanzoni," alisema Mapunda.

Alisisitiza kuwa, waliokuwapo kwenye mpango wa matumizi ya ardhi ambao ni takribani 145 walishaongea na NSSF na tayari walishakubaliana.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, Meneja Milki wa NSSF, Geofrey Timoth alisema katika kutekeleza maelekezo hayo ya Waziri wa Ardhi, NSSF inatarajia kuondoa nyumba zote ambazo zipo kwenye barabara na miundombinu ya maji pamoja na kuhakiki watu wachache ambao wanadai walikuwapo tokea mwaka 2021/22.

Timoth alisema kazi hiyo ni muendelezo wa utekelezaji wa maelekezo ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, aliyotoa wiki iliyopita.

Aidha, NSSF watakavyotekeleza maelekezo ya Waziri wa Ardhi ni kuwa bàadhi ya maendeleo yaliyofanywa ambayo waliyabaini mwaka 2021 na 2022 wamekubaliana kuwa watakaa na wahusika kwa sababu yapo kwenye mpango wa ardhi.

"Kwa hiyo tutakaa na wahusika na tutawaambia ni nini cha kufanya ili waendelee kuwa na amani kwenye maeneo husika," alibainisha Timoth.

Alisema kuwa maeneo ambayo yaliendelezwa nje ya mwaka 2021/22 yataenda kuondolewa kwa sababu NSSF ina mpango wa kuyaendeleza pamoja na utaratibu wa kuzuia uvamizi kwenye maeneo mengine.

KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Chuo chatakiwa kuboresha uchapishaji kiteknolojia

**Na Munir Shemweta,**
TABORA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amekitaka Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) kufanya maboresho kwenye sehemu yake ya uchapishaji ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia.

Pinda alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara katika chuo hicho ikiwa ni jihudi za kuhakikisha Chuo cha ARITA kinafanya kazi kwa ufanisi na kutoa huduma bora za uchapishaji.

Alisema, uboreshaji sehemu ya uchapishaji ndani ya chuo hicho kutakiwezesha kupata kazi nyingi za uchapishaji na kukiingiza pesa.

"Hivi vifaa mlivyokuwa navyo ni vya kizamani sana na haviendani na teknolojia ya sasa labda kama vitaendelea kubaki kwa ajili ya kufundishia wanafunzi ili kujua tulikotoka, lakini kwa kipindi hiki mnahitaji kuboresha ili muende sambamba na tekonolojia ya sasa," alisema Pinda.

Naibu Waziri ameutaka uongozi wa chuo hicho cha Ardhi Tabora kuandika gharama za vifaa vya kisasa ili akisaidie kupata vifaa vya kisasa vitakavyo kiwezesha chuo kuingia kwenye ushindani wa kibiashara.

Aidha, ameutaka uongozi wa Chuo cha ARITA kwenda kujifunza kwa taasisi nyingine ikiwamo ya Uchapishaji ya Serikali (Government Printers) ili kuimarisha sehemu hiyo na kufanya vizuri kwenye utendaji kazi wake.

"Chuo hakina Ofisa Miradi na lazima kiwe na watu wanaohitajika kama wataalamu wa usimamizi wa miradi hivyo lazima 'to change direction' (kubadili mwelekeo) hii ni biashara. Lazima kuwa na mtazamo mpya kuhakikisha mamlaka ya chuo inatoa matokeo. Mnaweza kuona kama mnakwenda, lakini mko katika mark time," alisema Pinda.

Awali, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora, Juma Mkuki, alisema chuo chake kinaendesha mafunzo pamoja na shughuli za uchapishaji kwa kushirikiana na wizara pamoja na wadau wengine na kinazalisha machapisho mbalimbali kwa idara za serikali, taasisi na mashirika mbalimbali kama sehemu ya kujiongezea kipato.

Kwa mujibu wa Mkuki, kuanzia mwaka 2019/2020 hadi sasa chuo kinazalisha machapisho ya nyaraka mbalimbali zinazotumiwa na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kumilikisha ardhi na usajili kwa ujumla.

"Chuo kinatoa huduma kwa taasisi zingine ambazo zinatumia baadhi ya machapisho yetu ikiwa ni pamoja na vitabu mbalimbali na nyaraka zisizo za kiserikali," alisema Mkuki.

Alisema, sehemu ya uchapishaji inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maabara kwa ajili ya uchapishaji.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizungumza na ujumbe wa Bank Of Africa Tanzania ulioongozwa na Mkurugenzi Mtendaji, Esther Cecil Maruma (katikati kulia) ulipomtembelea ofisini kwake jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# N. Waziri Mkuu aipongeza benki utoaji Bima ya Mifugo

**Na Mwandishi Wetu,**
BAGAMOYO

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameipongeza Benki ya NMB kwa kuanza kutoa bima ya mifugo inayolenga kupunguza hatari kwa wafugaji nchini.

Bidhaa hiyo ni sehemu ya dhamira ya benki hiyo ya kuwalinda wafugaji dhidi ya hasara za kifedha zinazoweza kutokea kwa wafugaji zikiwamo hatari za ghafla au zisizotarajiwa.

Akizungumza kwenye banda la benki hiyo wakati wa kufunga maonyesho ya siku tatu ya mifugo yaliyoandaliwa na Chama cha Wafugaji Kibiashara (TCCS) na kufadhiliwa na Benki ya NMB na kukutanisha na wadau mbalimbali wa sekta ya mifugo mwishoni mwa wiki, Biteko alisema kuwa bima ya mifugo ni dhana mpya katika soko la Tanzania na kuitaka benki hiyo kuongeza wigo wake ili kuwanufaisha wafugaji wengi nchini.

"Kwa kweli nimeifurahia hii dhana ya bima ya mifugo na nakiri kwamba ni dhana mpya katika soko la Tanzania," alisema.

Biteko alisema ingawa idadi ya ng'ombe imeendelea kukua siku hadi siku na kufikia milioni 37 katika miaka ya hivi karibuni, mchango wa sekta ya mifugo katika uchumi wa nchi bado ni mdogo sana.

"Hii ni kwa sababu ya kutegemea ufugaji wa ng'ombe wa kizamani. Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatakiwa kuja na mikakati mipya ya kuwawezesha wafugaji kubadili ufugaji na kuwawezesha kufuga kisasa," alisema.

Alisema tayari serikali imekamilisha Mpango Kabambe wa Sekta ya Kilimo unaolenga kutatua changamoto kadhaa zinazoendelea kukwamisha maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo nchini.

"Serikali ya awamu ya sita imedhamiria kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo," aliongeza.

Awali, Mkuu wa Idara ya Kilimo, Wateja Wakubwa ya Benki ya NMB, Christopher Mwalugenge, alisema bima ya mifugo inayotolewa na benki yake inajumuisha aina kadhaa za hatari zinazohusiana na mifugo, zikiwamo vifo na wizi wa mifugo.

"Kama benki, tunaelewa kuwa mifugo ni vitega uchumi muhimu hivyo ili kulinda wafugaji dhidi ya upotevu wa ghafla, tumekuja na hii bima mifugo ambayo inagharimu kiasi cha Sh. 20,000 tu kila mfungo kwa mwaka,"

Pia, benki yake imejikita kulinda vitega uchumi vya wafugaji kwa kutoa bima ya mifugo iliyoboreshwa ili kupata mustakabali wa mifugo yao pamoja na mustakabali wa biashara zao.

Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, wakati wa hafla hiyo aliwataka wafugaji kuachana na ufugaji wa asili na kuanza ufugaji wa kisasa ili kuleta tija katika biashara zao.

"Kama wizara, tumekuwa tukitoa elimu na kuhamasisha wafugaji kuachana na ufugaji wa kizamani na kuanza kufuga kisasa, lakini mwitikio bado ni mdogo sana. Wafugaji wengi nchini Tanzania wanaendelea kutegemea ufugaji wa asili ambao unadhoofisha tija. Siku zimepita ambapo mfugaji anasafiri umbali mrefu kutafuta malisho," alisema.

# Viongozi waaswa kuendelea kuombea amani nchini

**Na Steven William,**
MUHEZA

KATIBU wa Msikiti Mkuu wa Ijumaa wilayani Muheza Tanga, Shekhe Mohamed Baghoza, amewahimiza viongozi wa dini kuendelea kuombea amani katika taifa na kukemea vitendo vya uhalifu na ukatili wa kijnsia kwa watoto katika jamii.

Kauli hiyo aliitoa jana katika ibada ya swala ya Sikukuu ya Eid Elhaj, iliyofanyika katika msikiti mkuu wa Ijumaa wilayani hapa na kuongozwa na Imamu Omari Athuman Zuberi.

Swala hiyo iliyohudhuriwa na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Mohamed Mfaki na kuambatana na kisomo cha kuwaombea marehemu kilichoandaliwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini, Balozi Adadi Rajabu.

Baghoza alisema jamii yoyote inayolelewa na kukua katika misingi ya kufuata maandiko ya Mwenyezi Mungu ni vigumu kujiingiza kirahisi katika vitendo vinavyomchukiza Mungu vikiwamo vitendo vya uhalifu.

Aliwatakia heri waumini wote wa dini ya kiislamu kote nchini katika kusherehekea sikukuu ya kuchinja ya Eid Alhaji.

Balozi Adadi aliwashukuru Waislam pamoja na wananchi wa Muheza kwa kushiriki dua ya kuwaombea marehemu familia yake katika makaburi ya kijiji cha Kerenge pamoja na kupata sadaka ya chakula.

Alisema kitendo hicho cha dua ya kuwakumbuka marehemu hufanyika kila mwaka kila sikukuu ya Eid Elhaji kwa kukaribisha watu wote kufanya kisomo cha dua nyumbani na makaburini.

Aliipongeza serikali kwa hatua inazochukua kukabiliana na vitendo vya uhalifu nchini na kusisisita kuwa viongozi wa dini wataendelea kushirikiana na serikali kukemea vitendo viovu katika jamii kama hatua ya kuhakikisha vitendo vya uhalifu vinakoma nchini.

Balozi Adadi alitoa rai kwa viongozi wote wa dini na wananchi kudumishe amani, umoja, upendo na mshikamano miongoni mwao ili kuleta umoja na maendeleo na Muheza isonge mbele.

## Deni la bilioni 3/- bado kaa la moto H'shauri Arusha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Arusha, Missaile Musa, amesema serikali mkoani hapa, haitaifumbia macho Halmashauri ya Jiji hilo endapo itashindwa kujibu hoja 10 za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ikiwamo deni la Sh.bilioni 3.55.

Hoja nyingine inayoitikisa Jiji la Arusha ni ya mapato ya Sh. bilioni 2.1, ambayo hayajakusanywa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Missaile aliweka wazi juu ya msimamo wa serikali kuhusiana na hoja zinazoikabili Jiji hilo jana, wakati wa mkutano maalumu wa baraza la madiwani ulioketi kujadili hoja za CAG kwa mwaka 2022/23.

Aidha, alisema mwaka ujao wa fedha Mkoa wa Arusha utakuwa bega kwa bega kuhakikisha unafuatilia miradi yote na ukusanyaji wa mapato kwa Jiji la Arusha na pia ameagiza waache tabia ya kumwachia mweka hazina kujibu hoja peke yake bali kila mhusika ajibu hoja na kuzijua ikiwamo viambatanisho.

"Nina agiza Halmashauri ya Jiji la Arusha, kujibu hoja zote 10 za CAG ikiwamo ile ya deni ya Shilingi bilioni 3.55 pamoja na Sh.bilioni 2.1 ambayo haikukusanywa hivyo shirikianeni wote kujibu hoja na siyo kumwachia mweka hazina peke yake," alisema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji hilo, Juma Hamsini, alisema halmashauri hiyo imepata hati isiyo na shaka kwa mwaka wa fedha 2022/23 ikiwamo kutekeleza hoja 23 kati ya 49, ambapo hoja 23 zimetekelezwa na kubaki na hoja 26 ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

"Lazima madeni ya nyuma yakusanywe, lakini tutasimamia ulipaji wa madeni kwa kutumia POS mashine ili kuhakikisha madeni ya nyuma yote yanakusanywa sambamba na kuboresha mifumo ya ukusanyaji kodi ili fedha na miradi iliyopangwa ikamilike kwa wakati," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, aliwasisitiza watumishi kupunguza hoja zilizopo na hatimaye Jiji la Arusha kupata hati safi.

Licha ya kuzungumza hayo, alitumia fursa hiyo kuwapongeza watumishi wote wa halmashauri hiyo kwa ushirikiano wao uliosababisha Jiji hilo kupata hati safi.

Awali, Diwani wa Kata ya Sokoni, Saruni Olodi, aliomba mawakala wa ukusanyaji taka katika Jiji la Arusha, wanaodaiwa Sh. milioni 14.4 kupitia mashine za POS warudishe fedha hizo, kwa kuwa hadi sasa Sh. milioni 14.4 pekee ndio zimelipwa kama deni.

# Hali ya udumavu yamkera RC Sendiga, atoa maagizo

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SERIKALI mkoani Manyara imewataka wananchi kuchukulia takwimu za hali ya udumavu kwa watoto kama fedheha na aibu kwao, badala yake wapambane kukabiliana hali hiyo.

Mkuu wa Mkoa huo, Queen Sendiga, alieleza hayo jana, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyofanyika Wilaya ya Babati.

"Kutokana na hali ilivyo, nawahimiza kuhusu ulaji mzuri wa makundi yote matano ya vyakula kwa watoto na wajawazito. Kina mama watoto wetu kuwa na udumavu tuone fedheha, maana ni aibu tupambane ili kudhibiti hali hiyo. Lishe bora ni kinga kwa watoto hivyo inapaswa kuzingatiwa ili mtoto aweze kukua vizuri," alisema.

Katika maadhimisho hayo, baadhi ya wadau na watoto walishauri kuwa ili kulinda ustawi wa mtoto ni vizuri nchi wanachama kuangalia mifumo ya elimu, sera, utawala na mahakama inavyofanya kazi.

Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Galapo, Ally Juma, alisema mifumo hiyo ikitazamwa vizuri itatoa haki kwa watoto na kudhibiti udumavu na kuimarisha ulinzi kwa watoto.

Meneja Mradi wa Elimu wa Shirika la So They Can Tanzania, Grace Swai, alisema wao wanawajenga watoto kifikra ili wasirudi nyuma katika kudai haki zao.

"Elimu kuanzia chekechea ndilo jambo tunaliwekea msisitizo ili watoto wapate elimu bora, ndiyo maana tumewekeza kwenye miundombinu ya madarasa ya awali na mengine," alieleza Swai.

Aidha, alisema ili kuhakikisha mtoto anapata elimu bora wamewekeza kwenye miundombinu rafiki na wezeshi na mafunzo kwa walimu kuanzia ngazi ya chekechea na kusisitiza wazazi kuchangia uji kwa wanafunzi wa chekechea mpaka darasa la saba.



Baadhi ya waumini wa dini ya kiislamu wa mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wakishiriki swala ya Eid El Adha katika Msikiti wa Masjid Noor jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watoto yatima wapokea msaada vyakula

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Tanzanite Heroes Mining Camp ya Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, imetoa msaada wa vyakula kwa watoto yatima waliopo eneo hilo.

Msaada huo wa vyakula kwa watoto yatima walio chini ya miaka 14 ni pamoja na mchele, sukari, majani ya chai na mafuta ya kupitia na umegharimu Sh. milioni 2.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Heroes Mining Camp, Basil Roman Njau, akizungumza wakati akitoa msaada huo alisema hawajaanza kupata uzalishaji wa madini ila wametoa msaada huo ili iwe sadaka kwao.

"Mimi na mke wangu tumetoa kiasi hicho kwa ajili ya sadaka ya kusaidia yatima na endapo madini yatatoka mgodini kwetu tutawasaidia zaidi," alisema Njau.

Mwenyekiti wa Shirika la Saidia Wanajamii Tanzania (SAWATA), Mohamed Issa Mghanja alisema Mkurugenzi wa Kampuni ya Heroes Mining Camp, Basil Roman Njau ana moyo wa ukunjufu wa kusaidia jamii.

Alisema kwenye msaada huo wamewashirikisha wenyeviti wa vitongoji vyote ili kupata yatima wenye uhitaji halisi, hivyo wakawachukua wale wenye hali ngumu kabisa.

Aidha, alisema katika ugawaji huo wameshirikisha kaya 67 yenye watoto yatima 111 ambapo kwenye lita 140 za mafuta kila mmoja atapata lita moja, kila mtoto atapata kilo moja na nusu ya mchele na kilo moja na nusu ya sukari na paketi ya majani ya chai.

"Wajane wengine wana watoto wawili au watatu au wanne na kila mmoja atapata shea yake na mama zao watakula hapo hapo kupitia watoto wao," alisema Mghanja.

Alisema yatima wengi wa Mirerani wametokana na baba zao kufariki dunia kutokana na vumbi walilolipata kwenye shughuli za uchimbaji madini migodini.

Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani (TEO), Isack Mgaya, aliipongeza SAWATA kwa kusimamia zoezi hilo kwa uwazi na ushirikishwaji.

"SAWATA tumefanya nao kazi kwa muda mrefu bado ni asasi mahiri yenye uadilifu kwani kazi zao hazina kona kona zimenyooka na zinaaminika," alisema Mgaya.

Mmoja kati ya waliopatiwa msaada huo, Elizabeth John aliishukuru kampuni hiyo kwa kuwasaidia yatima hao ambao wengi wao wamewapoteza baba zao.

Alisema: "Kiasi hicho cha chakula kitawasaidia yatima hawa kwa muda wa siku kadhaa na tunawashukuru mno kwa moyo wa upendo mkubwa Mungu awabariki".



# Wazee kicheko, serikali ikiwahakikishia huduma

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WAZEE wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wamehakikishiwa kuwa serikali itaendelea kuwapatia huduma bora za matibabu bure.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, wakati wa uzinduzi wa Umoja wa Wazee Kata ya Masanga wilayani hapa.

Umoja huo uliasisiwa na Mkurugenzi wa Outreach Care International (OCI), Prof. Emmanuel Shija, ambaye ni mwenyeji wa Masanga.

Alisema serikali itakuwa pamoja na umoja huo, itaendelea kutatua adha mbalimbali zinazowakabili wazee wote wilayani hapa.

Alisema pia itaendelea kuwapatia huduma za matibabu bure kwa ajili ya kuimarisha afya zao.

Mkude aliwaomba wazee kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la makazi ili ifikapo siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu wajitokeze kwa wingi kwenda kupiga kura, kuwachagua viongozi makini wenye kuwaletea maendeleo na kupigania maslahi yao.

Katika hatua nyingine, alipongeza Kamati ya Maridhiano na Amani Mkoa wa Shinyanga kwa kuhakikisha amani inaendelea kutawala mkoani hapa pamoja na kumaliza tatizo la matukio ya mauaji ya yakiwamo ya wazee wilayani Kishapu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani, Mkoa wa Shinyanga, Shekhe Balilusa Khamis, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwashirikisha kwa kila jambo akisema hali ambayo imesaidia amani ya mkoa huo kuendelea kutawala.

Pia aliishukuru serikali kwa kukomesha mauaji ya wazee yatokanayo na imani za kishirikina, pamoja mimba na ndoa za utotoni zimepungua kulinganisha na miaka ya nyuma.


Mwekahazina wa Umoja wa Wazee Masanga wilayani Kishapu, Elizabeth Jimola, akisoma risala ya umoja huo, alisema ulianzishwa mwaka jana kwa kuasisiwa na Prof. Shija na sasa umoja una wanachama tisa.

Alisema malengo yao ni kuanzisha miradi ya kujikwamua kiuchumi, ili kuondokana na umaskini.

Alisema malengo mengine ya umoja huo ni kuhakikisha vijana wanakuwa na maadili, uzalendo na kulipenda taifa lao, kulinda na kudumisha amani ya nchi.

Kadhalika, alitaja lengo lingine ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuwaletea maendeleo wananchi.

Pia, aliipongeza serikali kwa kuendelea kuwajali wazee kwa kuwaboreshea huduma za matibabu bure, upatikanaji wa dawa, pamoja na kuwatengea madirisha ya kuwapatia huduma za afya na matibabu bila ya usumbufu.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, akikagua moja ya mashine ya uchapishaji ya muda mrefu kwenye Chuo cha Ardhi Tabora wakati wa ziara yake mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kaimu Mkuu wa Chuo, Juma Mkuki. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Watumia imani potofu kubaini maeneo yenye madini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu mkoani Shinyanga, wameliomba Shirika la Madini Tanzania (STAMICO), kufanya utafiti wa kiikolojia ili kubaini maeneo yenye madini ya kutosha.

Wamesema hali hiyo itasaidia kuondokana na njia inayotumika sasa ya mila potofu ya kupiga ramli chonganishi ili kutafiti madini katika maeneo hayo.

Walitoa rai hiyo wakati wa warsha ya elimu ya dhamana ya mikopo iliyofanyika wilayani Kahama iliyoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kushirikiana na STAMICO, ikiwa lengo ni kujikwamua kiuchumi na kunufaika na rasilimali hiyo.

Mmoja wa wachimbaji hao kutoka mgodi wa Mwimeilindi, Fadhiri Kipindula, alisema wamekuwa wakitumia imani potofu, katika kufanya utafiti wa ikolojia kwenye maeneo yaliyo na madini kwa kutumia mbuzi na kuku.

Alisema licha ya kutumia mbinu izo lakini bado hawapati madini ya kutosha, hivyo wanajikuta wanapoteza fedha nyingi kwa waganga wa jadi.

Alisema, STAMICO wakifanya utafiti huo katika maeneo hayo na kubaini madini yapo ya kutosha, wachimbaji hao watawekeza kukopa fedha na kuwekeza kwenye uchimbaji mkubwa, kuliko ilivyo sasa.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wadogo Shinyanga (SHIREMA), Hamza Tandiko, alisema ili kuondokana na adha hiyo ni vyema STAMICO wangefungua kituo cha utafiti wa madini.

Alisema kituo hicho kitakuwa kinafanya kazi hiyo mara kwa mara ikiwa na kutoa elimu kwa vitendo kuliko ilivyo sasa wachimbaji wanachimba kwa kubahatisha.

Alisema kila mchimbaji na mfanyabiashara wa madini anahitaji mkopo wa kuendeshea shughuli za uchimbaji kuliko hivi ilivyo sasa wanakopeshana wenyewe kwa wenyewe na wakati mwingine wanaweka dhamana ya nyumba.

Aidha, Ofisa wa STAMICO, Denis Silas, alisema hapo awali wachimbaji walikuwa wakifanya shughuli zao kwa kubahatisha, kwa sasa wamekuja na suluhisho la kufanya utafiti.

Alisema wana vifaa vya kisasa vya kuchoronga wakati wa kufanya utafiti, asilimia 16 ya maeneo yanayosadikika kuwa na madini wameyafikia na kuyafanyia utafiti na hivi karibuni wanatarajia kununua ndege ambayo itatumika kufanya utafiti, ili wachimbaji wachimbe bila kubahatisha.

Aidha, wakala wa huduma za serikali kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Sadick Nyanzowa, alisema serikali imekuja na mpango wa kuwakopesha wachimbaji wadogo fedha zinazotumika kukuza shughuli zao, jambo ambalo litawaondoa katika mikopo umiza.

Alisema wafanyabiashara wanaosafirisha nje watakopeshwa kwa muda wa mwaka mmoja kwa dhamana ya asilimia 75.

Pia wajasiriamali (wachimbaji) watakopeshwa kuanzia mwaka mmoja hadi mitano, kwa dhamana ya asilimia 50 na mikopo hiyo itatolewa na taasisi za kifedha na siyo BoT.

# Meya asisitiza utunzaji vyanzo vya maji, miundombinu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MEYA wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, amewasihi wananchi kutunza vyanzo vya maji na miundombinu, ili kuzuia upotevu wa maji waendelee kupata huduma hiyo kwa uhakika.

Alitoa wito huo wakati akizindua ligi ya Maji Cup, ambayo imeandaliwa na Taasisi ya Watoa Huduma za Maji (ATAWAS), yenye lengo la kutoa ujumbe kwa wananchi juu ya kutunza vyanzo vya maji, kuzuia upotevu na kutunza miundombinu ya maji.

Alisema maji ni uhai na bila maji hakuna maendeleo, hivyo aliwataka wananchi wajiepushe na kufanya shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji ikiwamo kilimo na uvuvi, ili vyanzo hivyo viendelee kuwapo na kusaidia upatikanaji wa maji muda wote.

Pia aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano pindi watakapoona mtu anaiba maji kwa kujiunganishia kinyemela kinyume na sheria watoe taarifa kwa mamlaka husika.

Pia aliwataka endapo wakiona kuna sehemu zinavuja maji watoe taarifa haraka ili kuzuia upotevu wa maji, huku akiipongeza SHUWASA kwa kuzuia upotevu wa maji kwa asilimia 17.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), Yusuph Katopola, alisema lengo la ligi hiyo ni kufikisha ujumbe kwa jamii juu ya kutunza vyanzo vya maji, kudhibiti upotevu wa maji na kutunza miundombinu ya maji.

Mtendaji Mkuu wa ATAWAS, Costantino Chiwaligo, alisema huu ni mwaka wa nne wanaandaa mashindano hayo ambayo hufanyika kila mwaka kwa kushirikisha timu za mamlaka za maji kutoka kanda 10.

Alisema baada ya hapo timu 32 ambao zitaibuka washindi kikanda watakwenda kucheza kitaifa jijini Dodoma ili apatikane mshindi wa jumla.

Alisema ligi hiyo ni wazo ambalo lilitolewa na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, mwaka 2021, ikiwa ni sehemu ya kampeni kwa ajili ya kufikisha ujumbe kwa wananchi kupitia michezo, kutunza vyanzo vya maji, kuzuia upotevu wa maji na kutunza miundombinu ya maji.

Alisema vyanzo vya maji visipotunzwa ikiwamo miundombinu ya maji pamoja na maji kupotea ni hasara kwa wananchi, sababu watakosa huduma ya maji na kusababisha mgawo.

"Kampeni hizi ni kuizindua jamii, kuwa maji yakipotea ni shida kwao sababu watakosa huduma ya maji, hivyo ni vyema wakavitunza vyanzo vya maji, kuzuia upotevu wa maji pamoja na kuacha wizi wa maji, sababu takwimu zinaonyesha upotevu wa maji asilimia 40 usababishwa na wizi wa maji, ikiwamo kujiuganishia kinyemela na kuchepusha maji," alisema Chiwaligo.

Aidha, alisema taasisi hiyo wapo kwenye hatua za kuanzisha mita za malipo ya kabla ili kuzuia upotevu wa maji, kwamba mchakato huo utaanza katika Mkoa wa Shinyanga.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 18, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 13

**SEO: Wazazi, walezi wasiwe chanzo cha watoto wao kuharibika, wawajibike**




Ukurasa 14

Watoto waonyeshwa mahali pa kudai elimu ikitokea wanaikosa



Ukurasa 12

Kilichojiri kwenye chimbuko la Siku ya Mtoto wa Afrika, 1976 Soweto, Afrika Kusini

NA GAUDENSIA MNGUMI

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

# Ndivyo anavyotishiwa kwa ukatili

• Sheria na adhabu zipo, zitumike kumlinda




Watoto wakishiriki maadhimisho ya Siku ya Mtoto Afrika. **PICHA: MTANDAO.**

KUWAELIMISHA watoto wawe bora na kuwa raia wanaofaa kwa karne ya 21 ndiyo kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka huu.

Ni tukio la kila mwaka linaloadhimishwa Juni 16 kwa heshima ya kuwaenzi na kuutambua mchango wa watoto walioshiriki maandamano Soweto Afrika Kusini mwaka 1976, kudai haki ya elimu kwa watoto weusi na kupinga ubaguzi wa rangi.

Watoto hao waliuawa kwa kupigwa risasi na maelfu kujeruhiwa.

Kaulimbiu mwaka huu, licha ya kutaka mtoto bora anayemudu maisha yake na anayefaa katika karne ya 21, ukatili na unyanyasaji wa watoto zama hizi unatosha kueleza kuwa kuishi kwa amani kwenye karne hii kunahitaji kumlinda zaidi mtoto.

Kinachozungumzwa kila kona leo iwe kesi mahakamani, shuleni, taasisi za kidini, mitaani na nyumbani ni ukatili dhidi ya watoto kuanzia kuwatumikisha kingono kwenye madanguro, ulawiti, ubakaj, mimba na ndoa utotoni, vipigo nyumbani na shuleni, kuwatumikisha kwenye kazi ngumu na kuwanyima haki nyingi hata chakula.

Mwezi uliopita Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni, anapowasilisha bungeni makadirio ya wizara kwa mwaka 2024/25, anasema makosa ya ukatili wa kijinsia yameongezeka na kwamba kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024, yameripotiwa polisi makosa 24,535 ikilinganishwa na 21,317 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23, ikiwa ni ongezeko la visa 3,218.

Anaonya kuwa ongezeko hilo linachangiwa na mmomonyoko wa maadili, hususan ubakaji na ulawiti wa watoto ambapo kesi 5,865 ziko mahakamani leo.

Ikumbukwe, haki za watoto zinalindwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na ule wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa 1990 yote Tanzania imeiridhia.

Taifa lina Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inayotaja haki zake zote na kusisitiza kumlinda, hata hivyo ukatili unatishia amani na hatma ya mtoto wa Tanzania.

Kwa mfano, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) katika ripoti zake kiliwahi kueleza kuwa watoto wa kiume wanafanyiwa zaidi ulawiti, suala linalokua kila mwaka, hufanyika shuleni, mitaani pia nyumbani.

Mathalani, kuanzia mwaka 2016 hadi 2021 pekee, kuna matukio 5,716 ya ulawiti wa watoto yaliripotiwa katika vituo mbalimbali. Watoto wanafanyiana ukatili wa kingono wao kwa wao ... katika maeneo mbalimbali kama mashuleni, njiani wanaporudi nyumbani nyumbani wanakiishi, inafafanua LHRC

“Ulawiti umekithiri, ni vyema kuwa makini na watoto wa kiume na kujua wanacheza na nani na nini wanachofanya, utandawazi umeharibu watoto.” Inaongeza ripoti ya LHRC, ya haki za binadamu.

Mambo yanayoonyesha kuwa watoto wanapitia wakati mgumu ni pamoja na kuwapo vibandaumiza vyenye burudani mbalimbali kama sinema, ngumi, kandanda na tamthilia ambazo huwavuta watoto na kulazimisha wakati mwingine kufanyiwa ukatili kingono.

Mfano, mwaka jana madanguro 700 yaliharibiwa mkoani Dar es Salaam, kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Hashimu Komba, akitangaza hayo, kwenye uzinduzi wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini.

Katika madanguro hayo, baadhi ya watoto hunyanyaswa na mambo hayaishii hapo wapo wanaovutishwa dawa za kulevya kama ‘kokein’ ‘mandaraks’, bangi , sigara, hata shisha na mwisho wa yote ni kudhalilishwa.

Mambo yote hayo yanawaumiza watoto wa Afrika wakiwamo wa Tanzania na kinachowapeleka kwenye dunia ya ajabu, ni kufundishwa na kuingizwa kwenye masuala ya ulawiti na ushoga ambayo licha ya kuifanya Afrika isiwe na watoto au vijana bora wanaofaa kwa karne ya 21, yanaongeza magonjwa kama VVU, homa ya ini na saratani za viungo vya uzazi.

**MAHALI PA KUANZIA**

Ili kuwalinda watoto na vijana wakuu wa mikoa na wilaya na kamati za ulinzi na usalama watii maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyowaagiza kuwalinda watoto na vijana ili wasiingizwe kwenye dunia ya sodoma na gomara ambayo ni tishio kwa usalama, afya na maendeleo ya taifa.

Katika moja ya mikutano yake na viongozi hao, anawataka viongozi hao na kamati za ulinzi na usalama kufuatilia watuhumiwa wanaotajwa pia mashirika ya misaada na kazi wanazofanya ndani ya maeneo yao.

Rais anaeleza kuwa miradi mingi yenye masuala ya mmomonyoko wa maadili inahusu huduma za afya, vijana na mazingira na kwamba ni eneo linalotakiwa kufuatiliwa na wakuu hao

INAENDELEA UK.12

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Ndivyo anavyotishiwa kwa ukatili

**INATOKA UK.11**



Namna yalivyokuwa maandamano ya watoto, Soweto, Afrika Kusini, hata kuzaa Siku ya Mtoto Afrika, tukio la mwaka 1976. . **PICHA: MTANDAONI.**

ili kudhibiti juhudi za kufundisha vijana watoto masuala yanayowapotosha.

Anawaambia kuwa dunia imeharibika na kwamba hata katika mikutano ya kimataifa viongozi wanaohutubia wanatangaza hadharani mfano mwanaume anasema nina mwenzangu akimaanisha kuwa yeye ana ndoa ya jinsia moja, kadhalika wanawake nao mwanamama anajivuna kwenye majukwaa ya kimataifa anapohutubia kuwa ana mwenzake na wako katika ndoa ya jinsia moja.

Anaeleza kuwa lengo la kufanya hivyo ni kuwazoesha watu duniani kuona na kukubali kuwa ni matendo ya kawaida ili dhana hiyo isambae na kukubalika miongoni mwa viongozi, wanajamii hasa vijana na watoto.

**SHERIA ZIFANYE KAZI**

Pamoja na kutii maelekezo, kulinda watoto na jamii, wakati umefika wa kutumia sheria kukataza na kukomesha uhalifu dhidi ya watoto na vijana, mfano Sheria ya Ndoa ya 1971 inazungumzia ndoa ya mke na mume, si vinginevyo, kama vile ndoa za jinsia moja.

Sheria ya Adhabu au 'Penal Code', Sura ya 15 inatoa adhabu ya kushiriki ngono kinyume na maumbile ambayo ni kifungo cha miaka 30 jela au cha maisha. Sheria hii itumiwe kumlinda mtoto na kijana wa Tanzania ili aishi na kuwa na maisha yenye tija.

Aidha, Sheria ya Makosa ya Kujamiiana itumiwe kuadhibu wanaowakatili watoto kwenye masuala ya ngono, mila na matendo potofu kama ngoma za vigodoro na kuwaingiza kwenye ndoa hata ukeketaji badala ya kuwaacha wasome na kuendeleza maisha yao.

Kama ambavyo wilaya za Ubungo na Kinondoni zilikomesha madanguro 700 na kuyavunjilia mbali, mikakati itumike kuwasaka wahusika wanaonajisi watoto shuleni, mitaani, vyuoni na kwenye taasisi za kidini na kuwafikisha mbele ya sheria.

**MAKONDA NI MFANO**

Viongozi wa taifa waliosimama kifua mbele kukataa ushoga na masuala yanayohusu mmomonyoko wa maadili ni pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Arusha Paul Makonda, aliyeazimia kukomesha mienendo hiyo Dar es Salaam, wakati huo akiwa anaongoza mkoa huo.

Ni mwaka 2018, Makonda aliwatangazia wakazi wa Dar es Salaam, kuwaripoti wanaotuhumiwa kujihusisha na ushoga ili wakamatwe.

> "Mathalani, pempasi na 'wipes' kwa watoto zinazoagizwa nje ni salama? Mafuta, dawa na hata 'toi' au 'midoli', mipira na vifaa vya michezo, vyakula na pipi wanavyopewa watoto ni salama?

Ni aina ya ujasiri, anaoufanya Rais wa Uganda Yoweri Museveni, na nchi hiyo haitaki kuendeleza jambo hilo linaloathiri afya, saikolojia, uchumi, maisha na hatma ya watoto na vijana wa Afrika wanaotakiwa kuwa 'fiti' kwenye karne ya 21.

Viongozi wengine wakisimama kama Makonda ambaye aliutikisa ufalme wa wanaohamasisha mienendo hiyo duniani hasa Marekani, Uingereza na Ufaransa ni mfano wa kuigwa katika vita dhidi ya nyoka huyo hatari anayeangamiza watoto na vijana Afrika.

Hata hivyo, kuna mamlaka kiserikali zilimkana Makonda na kueleza kuwa huo ulikuwa mpango wake mwenyewe wa kuwakamata watu wanaojihusisha na mambo hayo na kueleza kuwa siyo mkakati wake na kusema haihusiki.

Yote hayo pengine yalisababisha kudhoofisha juhudi ambazo kama zingeendelezwa tatizo hilo lingepunguzwa.

Pamoja na Makonda, wanahitajika mashujaa kama waziri mstaafu na mwanasheria mbobezi Dk. Harrison Mwakyembe, anayesimama kidete kutoa taarifa za mienendo inayoelekea kuiangamiza Tanzania, akiangaza kuwapoteza watoto shuleni kwa yasiyowafaa wakafundishwa.

Dk. Mwakyembe ameeleza mengi na kuzitaja taasisi zinazochagiza masuala hayo na kuomba serikali ichunguze na kuchukua hatua na kama ni mashirika ya misaada yakiwamo ya Magharibi

Kwa mujibu wa Dk. Mwakyembe kuna hoteli za Dar es Salaam, zimepewa zawadi na heshima kwa kuendeleza 'sodoma na gomora' .

Aidha, anasema yapo mashirika ya misaada ya kimataifa yanayofanya kazi hiyo shuleni tena za msingi na sekondari, vyuoni pamoja na miradi ya vijana. Ni vyema serikali iyafanyie kazi maelezo yake na kuwaokoa watoto wa Tanzania.

Anachokisema ni kwamba, taifa likomeshe, likatae misaada ya kuangamiza wananchi na lichukue hatua ikibidi kuwafukuza watuhumiwa wanaoshukiwa kufanya kampeni na kuiingiza nchi kwenye mambo yanayowaangamiza watoto na vijana.

Pia, anataja sheria zitumiwe kuwasaka na kuwafikisha mbele ya sheria wanahusika kwenye familia, asasi za kiraia, shuleni na popote kwa sababu sheria na adhabu zipo, tena zinazoyafanya matendo hayo kuwa jinai na haramu.

**UMAKINI UNAHITAJIKA**

Taifa linahitaji misaada lakini watoa misaada wasiachiwe sana wakasambaza dawa, vifaa tiba, glovu, huduma za uzazi wa mpango, kuwapa mabinti taulo za kike, mafuta na losheni za kujipaka maana hakuna anayejua kuna nini ndani yake.

Inawezekana kwa kufanya kazi zaidi, kuchunguza, kudukua na kufanya ujasusi wa kina kufahamu vitu vinavyotolwa vina nini hasa?

Mathalani, pempasi na 'wipes' kwa watoto zinazoagizwa nje ni salama? Mafuta, dawa na hata 'toi' au 'midoli' , mipira na vifaa vya michezo, vyakula na pipi wanavyopewa watoto ni salama?

Ni jukumu la mashirika likiwamo la viwango TBS kuchunguza kila kitu na kuujua ukweli. Pia, Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba (TMD), Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali zifanye kazi na kubaini siri zilizoko kwenye baadhi ya misaada kama dawa, mipira ya wanaume, ya kike, taulo za wanawake na vyakula.

Kadhalika, ni wakati sasa taifa litumie vyombo vyake kama; Polisi, Usalama wa Taifa, Uhamiaji, makachero, maofisa Ustawi wa Jamii na hata madakatari kuwachunguza, kuwafuatilia na kufahamu madhumuni na mienendo ya watu na taasisi mbalimbali za kimataifa na kitaifa zinazofanyakazi nchini ili kuliweka taifa kwenye ukanda wa usalama kimaadili na kiafya.

Suala la kuasili watoto nchi za Afrika ziliangalie mashirika ya kigeni yanakimbilia

Afrika kuifanya kuwa na idadi kubwa ya watoto wanaoasiliwa na wageni.

Afrika na Tanzania zijue kuwa kuasili Waafrika kunatokana na udhibiti mkubwa wa mpango huo katika mataifa ya Ulaya na Amerika Kusini, Afrika iamke nayo ikataze kwa sababu haijui lengo au lililojificha nyuma ya kuwaasili.

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

NA MWANDISHI WETU

# SEO: Wazazi, walezi wasiwe chanzo cha watoto kuharibika, bali wawahudumie



Matukio tofauti yanayomhusu mtoto na Siku ya Mtoto Afrika, Madaba, Ruvuma. **PICHA ZOTE: MTANDAONI.**

JUMAPILI Juni 16, taifa limesherehekea Siku ya Mtoto wa Afrika, inayolenga kuongeza ufahamu wa fursa, mafanikio, pia kuibua matatizo na changamoto za watoto wa Afrika na kuzitatua.

Ni katika maeneo ya malezi, maadili, afya, elimu na ulinzi wa watoto ambao leo wanakabiliwa na kuhusishwa na uhalifu, mmomonyoko wa maadili na kutumbukia kwenye utandawazi.

Katika juhudi za kuangalia na kuandaa hatma bora ya watoto, Asasi ya Kiraia ya Kuinua na Kuwezesha Jamii (SEO) ya Mkoa Dar es Salaam, inawagusa watoto wa Mtaa wa Kimara Matangini na kuwapa ujumbe wa upendo.

Hapo inawakusanya watoto kutoka kwenye familia, shuleni za awali na madrasa kuwaelimisha kuhusu chimbuko la Siku ya Mtoto wa Afrika na kuisherehekea.

Mkurugenzi Mtendaji wa SEO Upendo Mwinchande- Mungi, anasema aasisi yake imewaleta pamoja watoto, walezi na wazazi takribani 70, kumsherekea Mtoto wa Afrika na Tanzania kwa lengo la kukumbushana wajibu kwa watoto, hasa ulinzi na usalama.

Anaongeza kuwa ni fursa wanayoitumia kuwaelimisha ili wazazi wajitambua na kuwaandaa ili wawe watoto bora na wanyoofu,wafikie ujana wenye maendeleo na kujitegemea na baadaye uzee mwema unaolenga kuwa na Tanzania endelevu.

Akizungumza katika halfa hiyo inayofanyika Mtaa wa Kimara Michungwani Dar es Salaam, Upendo anasema iwapo wazazi na walezi watazingatia wajibu wa kuwalea watoto ipasavyo, Tanzania na Afrika italikwepa kama si kupunguza majanga yanayoumiza watoto.

Kadhalika anasema. tatizo la watoto la watoto wenye ukinzani na sheria, wahalifu, wengine wanaoishi kwenye mazingira na maisha magumu linaweza kudhibitiwa.

"Kama watapewa haki zao za msingi, kwa kupendwa, kulishwa chakula cha kutosha, mavazi na kupelekwa shule, kusingetokea watoto kusumbuka mitaani.

Tujue kuwa wanakimbia mitaani au kwenye uhalifu kutafuta vitu hivyo wanavyovikosa nyumbani, wanavyohitaji kupewa na wazazi au walezi." anaongeza.

Anafafanua kuwa matatizo yanayotokea kwa watoto leo, mengi chanzo ni wazazi na walezi kwani ndiyo wanaoyasababisha. Mfano, baba hasimamii wajibu wake, mama naye hajali majukumu yake na kuacha watoto kujilea.

Upendo anakumbusha kuwa, watoto wanaoonekana mitaani hawajazaliwa huko maana mtaa hauzai mtoto, akizitaka familia kuacha kuzembea malezi na kuhimiza kila mzazi na mlezi kumjali mtoto maana hakuna chenye thamani kuliko mtoto si mali wala dhahabu.

Aidha, anawaaambia washiriki kuwa SEO imewafundisha na itaendelea kuwafahamisha watoto kuwa wawazi na kufichua wanaowafanya ukatili na wasiogope kuwataja wahalifu ili wachukuliwe hatua.

Anazitaka shule kuwaelimisha watoto ili waufahamu unyanyasaji na kuwawezesha kujieleza kama wananyanyaswa ili wawe jasiri kusema.

"Wawekewe mazingira ya kusema kila matukio wanayokumbana nayo hasa ya ukatili ili wawe majasiri wa kuyapinga na kuyakwepr, wakatae na kupinga mambo yanayowaumiza na kuharibu maisha yao.

Kadhalika, Upendo anazitaka taasisi za kiraia, za kidini hata umma, kama ustawi wa jamii, ziwakumbushe wazazi na walezi kuhusu wajibu wao kwa watoto, hasa ulinzi na usalama wa watoto wao zama hizi za utandawazi wasiwaache kuzurura na kumezwa na makundi yanayowapotosha.

"Pamoja na hayo, tunahitaji kuwa na sheria ambayo itawakabili wale wanaomalizana kimya kimya na watu wanaofanya vitendo vya ukatili kwa watoto katika familia zao, wakiwamo ndugu wa karibu kwa lengo la kuficha siri."

Anasema, masuala ya kuoneana aibu au muhali yanasababisha watoto kuumizwa ndiyo maana wakati umefika wa kutaka kuwe na sheria hiyo.

### WAKUU WA SEO

Mtendaji Mkuu wa SEO, Neema Nyansuka, anawakumbusha wazazi wajifunze kuwa karibu na watoto wao na kujenga urafiki tena kuongea nao mara kwa mara, pia kuwachunguza kujua marafiki zao ni nani, wanapendelea kufanya na kila wakati wanakuwa wapi mfano msimu huu wa likizo.

"Usingojee mtoto wako afunzwe na dunia, imwambie habari za ngono, imfundishe kutumia dawa za kulevya, matendo ya ushoga, kutumia dawa za kuzuia na kutoa mimba, utoro shuleni, wizi," anasema Neema na kuongeza kuwa mwambie ajue hata akikutana nayo awe anaelewa na pia akuambie.

Anawashauri kutumia mbinu zote, ikiwamo kuwasiliana na wataalam wa saikolojia na malezi ili wawape ujuzi wa kuzungumza na kujenga urafiki na watoto wao wa kike na wa kiume.

"Kujenga urafiki ili kujua anachofanya na kuzuia wasipotoke kimaadili ni njia mojawapo ya kukabiliana na mmomonyoko wa maadili ulioko duniani sasa." anaongeza Mtendaji Mkuu Neema.

Rukia Dadi, ni Mwenyekiti SEO, ambaye katika sikukuu hiyo, anasema anatamani kuona wazazi na walezi wakijitambua na kulinda watoto na kuacha kujisahau kama ilivyo sasa.

Anatoa mfano kuwa, wapo watoto wanaoachiwa kuzurura kutwa hadi usiku mitaani si mzazi, mlezi au mwanafamilia anayewajali na kwamba katika mazingira hayo watoto wanapotoka.

Anawakumbusha kuwa ni vyema kujua kila wakati na kila hatua mtoto wako anayopitia ili umlinde, mfano usikae zaidi ya dakika tano au 10 bila kuuliza na kufuatilia mtoto wako yuko wapi.

Aidha, Rukia anaikumbusha serikali kuandaa sera ya familia, sheria na miongozo itakayofanikisha kuwa na usimamizi na ulinzi wa watoto na jamii dhidi ya mmomonyoko wa maadili kwenye malezi.

SIKU YA MTOTO WA AFRIKA

NA BEATRICE PHILEMON

# Watoto waonyeshwa mahali pa kudai elimu ikitokea wanaikosa

• Mzazi, mwalimu, polisi...wanaguswa mahali hapa




Wanafunzi wasichana mkoani Dar es Salaam, wakiwa kwenye maandamano kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA: MTANDAONI**.

UNAPOZUNGUMZIA haki ya elimu siyo wanafunzi au wazazi pamoja na walezi wote wanajua kuwa kila mtoto ni lazima kusoma awe anatoka kwenye kaya maskini, mwenye ulemavu, asiyeoona au yatima na anayeishi kwenye mazingira magumu.

Baada ya kugundua kuwa watoto wengi wanahitaji kusoma, lakini hawajui sehemu gani wanaweza kudai haki yao ya kupata elimu, asasi ya Women In Social Entrereneurship (WISE), kwa kushirikiana na polisi Kata ya Keko Mwanga B, Dar es Salaam wanawaonyesha wapi pa kwenda kudai elimu.

Ni mpango unaowanufaisha wanafunzi wa Shule ya Msingi Keko- Magurumbasi wa kupata elimu, kwa mujibu wa Inspekta wa Polisi, Kata ya Keko-Mwanga, Sospeter Oyuke.

Anasema mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha wanafunzi kujua maana ya haki ya elimu, sehemu gani wanaweza kwenda kuidai au kushitaki kama mzaz au mlezi akikataa kumsomesha mtoto au mwalimu akikataa kumfundisha shuleni.

Yanatolewa kwa wanafunzi wa Magurumbasi kama sehemu ya kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Afrika ambayo uadhimishwa kila mwaka Juni 16.

Anasema mwaka huu kauli mbiu ni : 'Educate an African fit for 21st century: Building resilient education system for increased access to inclusive long life, quality and relevant learning in Africa.'

Inayoweza kutafsiriwa "Kuelimisha Mwafrika bora anayefaa kwa karne ya 21: Kujenga mfumo wa elimu himilivu na kuwezesha sote kufikia maisha marefu na kuwa na mafunzo bora Afrika."

Wanafunzi 500 wamenufaika na elimu hiyo inayotolewa na polisi kwa kushirikiana na shirika la kimataifa la Holt Children's Services Incorporation kutoka Korea Kusini, anasema Oyuke.

"Jamani hakuna mlemavu, mtoto asiyeona kwenye kupata elimu, kila mtu ana haki ya elimu, mzazi au mlezi ukimwambia kuwa unataka kusoma, halafu akakataa kukosemesha unatakiwa kwenda kumshitaki au kutoa taarifa serikali ya mtaa, kwa ofisa maendeleo ya jamii ya kata au kituo cha polisi kilicho jirani," anasisitiza Oyuke

Mbali na hilo, mwalimu akikataa kuwafundisha wanamshitaki kwa mwalimu mkuu, mratibu wa elimu kata, ofisa elimu kata au kituo cha polisi chochote kilicho karibu nao ili waweze kuchukua hatua au mwalimu mkuu kuwapa mwalimu mwingine.

Pia ili kufikia ndoto lazima wasome kwa bidii, wawe na maadili shuleni, wachukie ukatili, wasijiingize katika mahusiano ya kingono katika umri mdogo kwa sababu huo ni sehemu ya mmomonyoko wa maadili.

"Watoto zama hizi wana matatizo ya maadili wakumbuke hawawezi kufanikiwa katika maisha iwapo watashiriki ngono katika umri mdogo, mabinti hupata mimba za utotoni, magonjwa ya ngono kama vile VVU na kushindwa kutimiza ndoto zao," anasema Oyuke.

Anaongeza kuwa ameamua kuwafundisha watoto baada ya kugundua kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wa shule za msingi zilizoko Keko Mwanga B na maeneo mengine hawajui kudai haki ya elimu kutoka kwa mzazi , mlezi au mwalimu kama wakiona imekiukwa au imevunjwa.

**UKATILI BINAFSI**

" Mtoto elimu inaanzia kwako, unatakiwa uwe na elimu zaidi ya darasani, kutambua ukatili unaokuzuia kwenda shule, ujisikie mwenyewe kwenda kusoma wala mtu asikukatili."anasema Oyuke.

Mtoto anawajibu wa kusoma kwa bidii na unapogoma kwenda shule ni kutojithamini na kujiuliza unategemea kuwa nani baadaye? Jitahidi kujithamini, usome kwa bidhii na ujue unachotaka kuwa hapo baadae, anasisitiza.

Ili kuondoa uhalifu lazima kupata wataalamu wanaoweza kufanya kazi katika sekta mbalimbali jukumu linaloanza na kuhakikisha mtoto apate elimu bora kuanzia ngazi ya chini.

Kwa upande wa watoto wa kike, kama mnapopata changamoto mfano vijana wanawahadaa wavute hadi kwa waalimu, ambao wana wajibu wa kuwalinda wakiwa shuleni.

Anawaambia wakitoka nje ya shule ni wajibu wao kujilinda na kuongeza kuwa wanataka watoto wa kike wasome waweze kutimiza ndoto zao kama ilivyo kwa mtoto wa kiume.

Vaileth Godwin , Meneja Mradi wa WISE, anasema ni haki ya mtoto na mzazi anapompeleka shuleni, anatakiwa kusoma kwa bidii, kushinda vitu kama vishawishi, uvivu, makundi mabaya, utoro, dawa za kulevya na matukio kama ya , vigodoro ili kufaulu na haki ya elimu itakuwa imekamilik.

Anasema, ndiyo lengo la kuwahamasa watoto kusoma kwa bidii na kufanya vizuri bila kujali mazingira waliyonayo hasa Keko ambako mwamko wa elimu ni mdogo mno.

Mbali na hilo anasema katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika jamii inapaswa kutambua ,kuheshimu na kulinda haki za watoto kwa kuzingatia kwamba zimekuwa hatarini mfano kufanyiwa vitendo vya ubakaji, mimba na ndoa za ututoni na ukatili wa kimwili, anasema .

Vaileth anaonya kuwa vitendo vyote hivyo vimekuwa vikifanywa na ndugu wa karibu wa watoto na kusababisha ugumu wa kuwachukulia hatua za kisheria kwani masuluhisho mengi huishia kwenye familia na wakati mwingine hakuna anayetaka kutoa ushahidi kwa kuoneana aibu.

Anaongeza kuwa watoto wakielewa haki zao na kuzijua wanaweza kuchukua hatua na kuwapa elimu hiyo kwa wanafunzi wanoishi kwenye kata hiyo baada ya kugundua kuwa wengi wanaishi kwenye mazingira magumu.

Pia, wazazi wengi katika eneo hili hawajali na hawaelewi namna ya kulea watoto na huwaacha wajilee wenyewe yaani hawafuatilii watoto na hii ndiyo inasababisha watoto kutojua wapi anaweza kwenda kudai haki yake.

Anasema WISE imeamua kuanzisha programu hiyo kutokana na takwimu kuonyesha kwamba watoto wengi wa Keko Mwanga B wanaacha shule na wengine wanachelewa kuanza shule kwa sababu ya kukosa mahitaji ya shule chakula na gharama za matibabu.

Aidha, anatoa wito kwa serikali za mitaa, maofisa maendeleo jamii kata na polisi kwa kutambua kuwa wajibu wa kulinda na kutetea maslahi ya mtoto katika maeneo yao.

Vaileth anatoa wito kwa serikali za mitaa kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuwatafuta wazazi, walezi na ndugu wa watoto waliotelekezwa kwa nia ya kuwapata ili wawahudumie watoto malezi yaliyojengwa katika misingi bora .





## Matukio ya ubakaji, ulawiti yakithiri Dodoma

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Polisi Jamii Mkoa wa Dodoma Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP), Eva Stesheni, amesema takwimu za mwaka 2023 zinaonesha kuwa makosa ya ubakaji mkoani Dodoma yaliyoripotiwa ni 250 na kati ya hayo ya ulawiti yalikuwa 92.

Aliyasema hayo jijini Dodoma kwenye mkutano ulioandaliwa na Kanisa la Tanzania Fellowship of Churches (TFC) kwa niaba ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, SACP Theopista Mallya, uliofanyika katika viwanja vya kisasa.

"Kama mnavyoelewa makosa haya mara nyingi yanamalizwa kimya kimya kwenye jamii, kwa hiyo ukipiga hesabu ya kawaida ni kwamba inawezekana mengi zaidi yanatokea Jiji la Dodoma," alisema.

Alisema kumekuwa na ukatili wa kijinsia wa namna hiyo, kutokana na matendo maovu yanayojitokeza ikiwamo kuongezeka kwa ulevi katika jamii, imani za kishirikina, hasira zilizopitiliza, elimu duni ya malezi kwa wazazi na yenyewe inaongeza ukatili wa kijinsia.

"Ubize tunaokimbizana nao, sayansi na teknolojia tuliyonayo sasa hivi inachangia watoto wetu kukaa katika mazingira ambayo siyo mazuri.

"Mungu aliumba familia mpango wake ulikuwa kwa mtu mume na mke kuoana milele na kuwalea watoto kwa kujua na kumheshimu yeye akaleta familia Adamu na Eva wawe na familia wawe na watoto," alisema.

Kadhalika, aliwataka wananchi kudhudhuria mikutano inayoandaliwa na viongozi wa dini ili kusikia neno wanaloenda kulihubiri na kulifundisha ili kuondokana na vitendo vya maovu.

Akizungumzia kwenye mkutano huo, Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Fellowship Of Churches (TFC), Dk. Godfrey Malassy, alisema kuwa kuna injili ambazo zinatembea ambazo siyo za kweli.

Alisema injili hizo zinaleta mkanganyiko mkubwa kwenye jamii na wakati mwingine imefikia mahali kanisa linakosa namna ya kuheshimika kimaadili.

"Biblia iko wazi kwamba injili inatolewa bure, maombi yanatolewa bure sicho tunachokiona leo, leo hii maombi yanauzwa unaambiwa ugonjwa wako ni maombi gharama yake ni Sh. 50,000 sasa mwananchi wa kawaida ambaye hana uwezo atapata wapi," alisema.

Alisema, Yesu alikuja kwa sababu ya watu wenye shida na hakuwahi kufanya kitu cha namna hiyo na wala hatuna mstari hata mmoja kwenye Biblia unaonyesha kuna mtumishi yeyote aliyeandikwa kwamba wameuza maombi, wameuza mafuta, wameuza maji, wameuza chumvi," alihoji.

Hata hivyo alitoa wito kwa jamii kuitikia yale yanayoaswa na yale yanayofundishwa ambayo ni ya kweli.

# Jaji Kiongozi aagiza 'speed' usikilizaji wa mashauri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Mustapha Siyani, amewaagiza majaji wapya wa mahakama hiyo walioapishwa mwishoni mwa wiki, kuanza kazi kwa kasi sambamba na kuunga mkono matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili kurahisisha utendaji kazi zao.

Alitoa agizo hilo wakati akizungumza na majaji hao ofisini kwake jijini hapa, kuwaeleza kuwa anatarajia waanze kazi kwa kasi ikiwamo matumizi ya TEHAMA.

"Natarajia muanze kazi kwa kukimbia, muwe kama askari wanaoshuka chini na parachuti ambao mwendo wao hata baada ya kushuka chini ni wa kasi, hivyo muwe wepesi kujifunza kwa haraka ili tuweze kusonga mbele," alisema Jaji Siyani.

Alisema majaji hao wameanza kazi wakati mzuri ambao ni katikati ya mwaka, hivyo ni rahisi kuwapima katika kipindi hiki cha miezi sita iliyobaki kuhitimisha mwaka.

Aidha, alisema ongezeko la majaji hao anaamini kuwa litaenda sambamba na uharaka wa upatikanaji wa haki kwa kuwa mzigo wa mashauri kwa majaji wa mahakama unaendelea kushuka.

"Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2023 wastani wa mzigo wa mashauri kwa kila jaji ilikuwa ni 307, hivyo ongezeko la majaji wapya wanne pamoja na mwingine aliyeapishwa Aprili litapunguza mzigo wa mashauri kwa kila jaji na kufanya kuwa 298," alisema Jaji Kiongozi.

Kadhalika, aliwaasa majaji hao kuzifahamu na kuziishi kanuni za maadili za maofisa mahakama.

"Mmeshakuwa majaji, kuanzia sasa mjue nyendo zenu zinafuatiliwa, mnapaswa kuyaishi maisha yanayoakisi maadili, tupo kwenye zama ambazo kosa moja tu linaweza kuharibu taswira ya mahakama nzima," alisisitiza.

Aliongeza kuwa, kiongozi siyo tu hapaswi kukiuka maadili lakini hapaswi kutiliwa mashaka ya kutokuwa na maadili, hivyo ni muhimu kuzingatia hayo pamoja na kuziishi tamaduni mbalimbali za mahakama.

Vile vile, aliwataka majaji hao kufanya kazi vizuri na watumishi walio chini yao, ambapo alisema: "Mnalo jukumu la kulea wasaidizi walioopo chini yenu, mnapaswa kuwaandaa kuwa watu ambao watapokea vijiti vyenu kwa kuwa nchi ya kesho yetu inategemea sana kizazi tunachokiandaa sasa."

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma, Dk. Juliana Masabo, aliwasihi majaji hao kufanya kazi kwa kumpendeza Mungu kwa kuwa nafasi hiyo ni ya kipekee.

"Kazi ya kuhukumu ni kazi ya Mungu, tunapaswa kufanya kazi hii kama Mungu anavyotutaka," alisema Dk. Masabo.


Aliwaomba majaji hao kushirikiana na majaji wenzao pamoja na manaibu wasajili, makarani na watumishi wengine ili utendaji wao uwe rahisi.

Dk. Masabo pia aliwasihi majaji hao kuwa tayari kujifunza ambapo alisema kuwa hawapaswi kuona aibu kuuliza au kupata ushauri kutoka kwa majaji wenzao juu ya namna bora ya kufanya vizuri zaidi katika kazi.

Majaji na Msajili wa Mahakama ya Rufani Tanzania pamoja na viongozi wengine wa serikali walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali walioapishwa mwishoni mwa wiki na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma.

Majaji walioapishwa ni Projestus Rweyongeza Kahyoza, Mariam Mchomba Omary na Nehemia Ernest Mandia.

Aidha, George Hillary Herbert naye aliapishwa kuwa Msajili wa Mahakama ya Rufani Tanzania.



Waumini wa dini ya Kiislam wakiwa katika ibada ya sikukuu ya Idd Al Adha, katika msikiti uliopo eneo la Msikitini, Mbezi Malamba Mawili Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wataka watoto wenye ulemavu kupewa haki sawa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKATI Tanzania ikiungana na mataifa mengine kusherehekea Siku ya Mtoto wa Afrika, wadau wa masuala ya mtoto wameiasa jamii kuhakikisha watoto wenye ulemavu wanapewa haki sawa na wengine bila kujali hali zao.

Mratibu wa Programu wa Taasisi ya Tanzania Foundation for Excellence in Disability (TFED), inayojihusisha na kutetea watu wenye ulemavu, Christina Mngara, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi wa watoto wenye ulemavu wakati wa maadhimisho ya Siku wa Mtoto wa Afrika.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuwajibika katika kutoa haki sawa za msingi kwa watoto hao wenye ulemavu ikiwamo elimu, matibabu, malazi bora, chakula na mavazi, badala ya jukumu hilo kuiachia serikali na wadau wa maendeleo peke yao.

Mngara, alisema wazazi, walezi na jamii wakiwajibika kwa pamoja kwa watoto wenye ulemavu ipasavyo bila kujali hali zao kwa kuwaendeleza vipaji vyao kwa usawa watawasaidia kubadilisha maisha yao.

Kadhalika, aliwataka wazazi, walezi na jamii kutumia nafasi zao kuwalinda na kuwaunga mkono watoto wenye ulemavu kwa kusimamia haki zao na maslahi, hali itakayowawezesha kuwa watu wenye uwezo na ujuzi pamoja na kujenga uzalendo kwa taifa lao.

"Hapa niwaombe wazazi, walezi na jamii kwa kuzingatia umuhimu wa Siku ya Mtoto wa Afrika, tunapaswa kuendelea kuhamasisha ujumuishaji wa watoto wote katika elimu na jamii kwa ujumla ili mtoto mwenye ulemavu awe na maandalizi ya maisha yake ya baadaye," alisema.

Naye Kaimu Ofisa Elimu Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi Dodoma Jiji, Tatu Mwangu, alisema kuwa serikali pamoja na wadau wa maendeleo yakiwamo mashirika yasiyo ya kiserikali, itaendelea kushirikiana na wazazi na walezi wenye watoto walemavu ili kuhakikisha mahitaji yao ya msingi yanawafikia kama ilivyo kwa wengine.





# Wafanyabiashara wataja sababu sukari kuuzwa ghali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA mkoani Mbeya wamesema bei ya sukari haiwezi kushuka ndani ya mkoa huo licha ya serikali kutangaza bei elekezi.

Wamesema hali hiyo inasababisha na vibali vilivyotolewa vya kuagiza sukari nje ya nchi kuelekeza iagizwe kutoka nchi za Ulaya na Brazil ambako wanatumia gharama kubwa kuifikisha mkoani humo.

Walitoa msimamo huo wakati wa mkutano wa Baraza la Biashara la Mkoa wa Mbeya uliofanyika ndani ya ofisi za mkuu wa mkoa huo.

Walisema hatua ya serikali kutoa vibali vya kuagiza sukari nje ya nchi kwa viwanda vya sukari nchini pekee na kuelekeza sukari hiyo iagizwe kutoka nchi za Ulaya na Brazil haikuzingatia mahitaji wala mazingira ya wakazi wa Mkoa wa Mbeya.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Julius Kaijage alisema kwa kiwango kikubwa wakazi wa Mkoa wa Mbeya na mingine ya jirani inatumia sukari kutoka nchi jirani za Zambia na Malawi lakini vibali vilivyotolewa na serikali haviruhusu sukari kuingia nchini kutoka kwenye nchi hizo.

Alisema endapo wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya watanunua sukari iliyoagizwa kutoka Ulaya na Brazil ambayo inaingizwa nchini kwa vibali halali vya serikali, wanatumia gharama kubwa kuifikisha mkoani Mbeya na hivyo kuiuza kwa bei ya juu kwa wananchi.

Kaijage alisema kuwa kwa sasa sukari inayotumika mkoani Mbeya inaigizwa kutoka nchi za Zambia na Malawi na kupitishwa katika njia za panya kutokana na kutokuwa na vibali vya sukari hiyo kuingia nchini.

Alisema kutokana na sukari hiyo kuingia nchini kwa njia za panya na yenyewe haiwezi kushuka bei kwa kuwa inaingia kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya wananchi.

Kwa upande wake, Prince Mwaihojo aliishauri serikali kutoa vibali vya kuingiza sukari nchini kwa kuzingatia mazingira ya maeneo husika na vibali hivyo wapewe wafanyabiashara badala ya viwanda vya sukari.

Akizungumza kwa niaba ya Ofisa Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Ofisa Mifugo wa Mkoa wa Mbeya, Samora Mshang'a, alisema Mkoa wa Mbeya hauna tatizo la uhaba wa sukari na badala yake tatizo lililopo ni bei kubwa ya bidhaa hiyo.

Alisema taarifa zilizokusanywa kutoka katika halmashauri zote saba za Mkoa wa Mbeya zinaonyesha sukari ipo ya kutosha lakini kero kubwa kwa wananchi imekuwa ni bei ya juu ya bidhaa hiyo.

"Taarifa zinaonyesha kuwa bei ya sukari katika halmashauri zetu zote saba ni kati ya shilingi 4,500 na 5,000 kwa kilo moja, bei ambayo ni ya juu ikilinganishwa na bei elekezi iliyopangwa na serikali," alisema Mshang'a.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kwenye baraza hilo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Benno Malisa, alisema jukumu la kuweka mazingira mazuri ya biashara mkoani Mbeya ni la pande zote mbili kwa maana ya serikali na sekta binafsi.

Alisema wafanyabiashara kwa upande mmoja na wao wanao wajibu wa kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara badala ya kuinyooshea kidole serikali.



Mshauri wa Rais Masuala ya Wanawake, Sophia Mjema (katikati) akifurahi na makundi ya kinamama wa Mkoa wa Iringa, wakati Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) lilipoifikisha Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA) mkoani humo. **PICHA: DAMAS MKANGALE**

## Mjema ataja faida Programu ya Imarisha Uchumi na Samia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI mkoani Njombe wametakiwa kutumia fursa ya Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia yenye lengo la kuwaunganisha na taasisi za fedha zinazotoa mikopo kwa riba nafuu, ili kuweza kujiinua kiuchumi.

Hayo yalielezwa mkoani Njombe na Mshauri wa Rais katika Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Sophia Mjema wakati wa mkutano wa kutambulisha programu ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Mjema alisema ili kuleta tija kila mwananchi anapaswa kushiriki kwenye programu hiyo.

Mjema alisema kila kundi linapaswa kushiriki katika uchumi sambamba na kuzalisha bidhaa na kuzisafirisha nje ya nchi.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Beng' Issa alisema baada ya usajili uliofanyika baraza hilo litakwenda kuchakata na kuona fursa za kuwasaidia wananchi.

"Tanzania tunakadiria kuwa na wajasiriamali milioni tano na asilimia 54 na hao ni wanawake kwa hiyo unaweza kuona ili eneo ni muhimu sana," alisema Issa.

Alisema kwenye eneo la matumizi ya ardhi kwa ajili ya uchumi serikali imeelekeza katika kupima ardhi kupitia programu ya kurasimisha ili kuweza kuitumia kwa ajili ya uchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka alisema hataki kuona wananchi wake wanakuwa maskini ili hali fursa zipo, hivyo kila mmoja anapaswa kujituma kuzichangamkia.

# TARI yakamilisha utafiti wa mbegu mpya ya ulezi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole cha jijini Mbeya, imekamilisha utafiti wa aina tisa za mbegu za ulezi ambazo zinatarajiwa kupelekwa katika Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI), kwa ajili ya kuthibitishwa ili zianze kusambazwa kwa wakulima.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Dennis Tippe, aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya Siku ya Mkulima wa Ulezi yaliyofanyika kwenye shamba la utafiti wa ulezi lililopo kituoni hapo, ambayo iliambatana na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kilimo bora cha zao hilo.

Alisema utafiti huo unalenga kuongeza tija ya uzalishaji wa zao hilo pamoja na kuboresha lishe kwa wananchi kwani zao hilo linachukua nafasi kubwa kwenye utengenezaji wa lishe za watoto na makundi maalumu ndani ya jamii.

Alisema wameamua kufanya maboresho ya utafiti wa mbegu za ulezi baada ya kubaini kwa muda mrefu zao hilo halijapata msukumo katika utafiti na kuliendeleza licha ya umuhimu wake kwa ajili ya matumizi ya lishe na usalama wa chakula.

"Sasa hivi mahitaji makubwa ya wakulima ni kupata mbegu bora na mbegu sahihi na kama kituo tunafanya utafiti kwa hatua tofauti tofauti, kwa hiyo mbegu hizi zitasaidia kuongeza tija ya uzalishaji wa ulezi na wakulima watapata mbegu hizo kwenye vituo vyetu vyote," alisema Dk. Tippe.

Ofisa Kilimo kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Benard Libata, alisema zao hilo limekuwa na msukumo mdogo kwa jamii licha ya umuhimu wake, hivyo baada ya kupata elimu kwa kushirikiana wakulima wengine watakuwa mabalozi wazuri wa kuhamasisha kilimo cha ulezi katika maeneo yao.

Katibu Tawala Wilaya ya Mbeya, Mohamed Fakii, aliwataka wakulima kuchangamkia kilimo cha ulezi kama zao la chakula na biashara ikizingatiwa na mabadiliko ya tabia nchi yanayojitokeza mara kwa mara kwani zao hilo linahimili ukame.

Mmoja wa wakulima wa ulezi, Caroline Mwakalambile, alisema wamejifunza kupitia shamba darasa namna wanavyoweza kuzalisha kwa tija zao hilo.





# Wananchi wapewa tahadhari ugonjwa wa kuhara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imetoa tahadhari kwa wananchi kujikinga na magonjwa ya mlipuko, kwamba hivi sasa kuna ongezeko la wagonjwa wa matumbo ya kuharisha katika vituo vya afya na hospitali.

Tahadhari hiyo imetolewa na Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, akisema ugonjwa huo husababishwa na uchafu unaosababishwa na kunywa au kula vimelea vinavyopatikana katika maji au chakula kilichochafuliwa.

Alisema kutokana na ongezeko la magonjwa hayo ni vyema wananchi wakachukua tahadhari haraka hasa katika kipindi hiki cha kusherehekea Sikukuu ya Iddi.

Mazrui alisema Wizara ya Afya inatoa mwongozo wa uuzaji wa vyakula na vinywaji katika viwanja vya kusherehekea Sikukuu ya Iddi na maeneo mengine ya Unguja na Pemba.

Pia aliitaja baadhi ya miongozo hiyo ni kuhakikisha wafanyabiashara wote wa vyakula kuwa na ndoo zenye mifereji (bomba) na sabuni kwa ajili ya kunawa mikono, kuosha vyombo kwa maji tiririka na sabuni baada ya matumizi na kabla ya kutumia tena.

Alisema pia wanapaswa kutunza usafi wa mazingira katika maeneo ya biashara sambamba na kudumisha usafi wa mwili.

Alisema Juisi hairuhusiwi kuuzwa kwenye viwanja vya sikukuu na wafanyabiashara wote kufuata kanuni, masharti na taratibu za biashara ya chakula ili kumlinda mteja na maradhi.

Mazrui alisema ukaguzi utaendelea kufanyika katika viwanja vyote vya kusherehekea sikukuu na maeneo mengine ya biashara za vyakula, kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka ikiwa ni pamoja kufungiwa kufanya biashara.

"Wizara ya Afya inawataka wananchi wote kuchukua hatua za kujikinga na magonjwa ya matumbo na kuharisha kwa kunawa mikono kwa maji tiririka kwa sabuni kabla ya kula, baada ya kutoka chooni, kunywa maji yaliochemshwa au yaliowekwa dawa ya kutibu maji, kuepuka kula chakula kilichopoa au kilichoandaliwa katika mazingira machafu na kuosha matunda kabla ya kula," alisema.

Pia, aliwataka wananchi kuepuka kutupa taka ovyo na katika maeneo yasiyo rasmi, kuwataka wananchi kuchukua tahadhari kwa kujikinga na magonjwa ya mlipuko kwa sababu kinga ni bora kuliko afya.

# SMZ , Saudi Arabia kushirikiana uendeshaji wa shughuli za Hijja

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema kuwa tayari makubaliano yameshafikiwa kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Saudi Arabia ya kuwa na akaunti mbili katika uendeshaji wa shughuli za hijja, chini ya ofisi moja (Biitha) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika Baraza la Iddi lililofanyika Micheweni Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema pia Shirika la Ndege la Saudi Arabia mwakani litaanzisha safari za moja kwa moja kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, kwamba kuanza kwa safari hizo kutawapa fursa mahujaji kusafiri kwa wepesi na kwa gharama nafuu.

Alisema katika utekelezaji wa dhamira ya serikali ya uanzishaji wa mfuko wa hijja nchini na kuwawezesha waislamu wengi kupata fursa ya kwenda kutekeleza ibada, serikali tayari imepokea ripoti ya kamati ya wataalamu ya kuimarisha kamisheni ya wakfu na mali ya amana.

Dk. Mwinyi alisema mapendekezo ya ripoti hiyo ambayo utekelezaji wake utaanza hivi karibuni yamezingatia upeo mkubwa wa shughuli za taasisi hiyo zikiwamo uanzishaji na usimamizi wa mfuko wa hijja.

Alisema pia itazingatia usimamizi wa fedha za zaka, uratibu wa baytul mali, umra na ziara kwenye maeneo ya historia ya uislamu au utalii wa kiislamu.

Kadhalika, Dk. Mwinyi alisistiza umuhimu wa kuyaendeleza mafunzo yanayotokana na ibada mbalimbali katika maisha ya kawaida hususani suala la kuhimizana kufanya mambo mema na kukataza mambo mabaya.

Alisema Wazanzibari wanasherehekea sikukuu hiyo wakati nchi ipo katika harakati za utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo Unguja na Pemba, kwamba serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ya sekta ya elimu, ujenzi wa miundombinu na huduma nyingine za jamii.

Alisema pamoja na miradi hiyo inayoendelea katika sekta ya elimu, hivi karibuni serikali itaanzisha ujenzi wa jengo la Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Tumbe na ujenzi wa dakhalia katika Chuo cha Kiislamu Micheweni.

Alisema kuhusu miundombinu ya barabara, serikali inaendelea na utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa barabara za ndani kwa hatua mbalimbali pamoja na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika maeneo huru ya uwekezaji Micheweni.

Alisema hatua za ujenzi wa Barabara ya Chake - Wete kwa kiwango cha lami unaendelea pamoja na ujenzi wa Bandari ya Shumba.



Mchuuzi wa mbuzi, Ramadhan Abdallah, akiwa amembeba kwa ajili ya kumpelekea mteja wake katika Soko la Mbuzi Vingunguti jijini Dar es Salaam jana, mbuzi mmoja aliuzwa kuanzia Sh.120,000 hadi Sh.200,000. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# M/kiti CCM: Wasaidieni wasiojiweza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mjini, Talib Ali Talib amewataka viongozi na watu wenye uwezo kujumuika katika kuwasiadia wananchi wasiojiweza hasa katika kipindi hiki cha Sikukuu ya Idd.

Alitoa wito huo jana visiwani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutoa sadaka ya chakula kwa wananchi na wanachama wa mkoa huo katika kusherehekea sikukuu hiyo.

Alisema kitendo cha kutoa sadaka kwa kuwasaidia watu mbalimbali hasa wasiyo na uwezo au wenye kipato kidogo kinajenga umoja, upendo na mshikamano.

"Unapokaa na wenzako ni jambo zuri na kuwasaidia wale ambao wasio na uwezo na jambo hili linajenga upendo katika nchi yetu," alisema.

Alisema haipendezi kufanya israfu ya chakula, hivyo ni vyema kuwagaia na wale ambao hawana uwezo kuliko kutupa au kumwaga chakula wakati wapo wanaokihitaji.

Baadhi ya wananchi waliopata sadaka hiyo ya chakula walisema kuwa sadaka hiyo imekuja muda mwafaka ambapo itasaidia kupata mlo mzuri katika kipindi hiki cha sikukuu.

Ali Haji alisema: "Tunamshukuru sana kwa hiki alichotupa siyo kwamba anauwezo mkubwa lakini ameamua hicho kidogo alichonacho kutukumbuka na sisi tunawaomba viongozi wengine na watu wenye uwezo kuiga mfano wake".

Alisema katika utoaji wa sadaka hiyo ya Mwenyekiti wa CCM haikuwa na ubaguzi wa kidini, chama wala ukabila na kila mmoja kapata sadaka hiyo ili kujumuika pamoja katika kusherehekea sikukuu.

# HABARI PICHANI



Kadhi wa Mkoa wa Iringa, Abubakar Chalamila, akitoa mawaidha ya Eid baada ya Swala ya Eid Al Adha iliyofanyika jana Uwanja wa Samora mjini Iringa kwa waumini wa dini ya Kiislam. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Katibu wa Sekretarieti ya Baraza la Ulamaa Taifa, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Shekhe Suwed Twaibu, akitoa mawaidha wakati wa swala ya Eid Al Adha iliyoswaliwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waumini wa dini ya Kiislamu wakiswali katika ibada ya sikukuu ya Idd -El - Adha iliyofanyika Msikiti Mkuu wa Gadaff Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**



Katibu wa Sekretarieti ya Baraza la Ulamaa Taifa, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Shekhe Suwed Twaibu (kulia), akitakiana heri ya sikukuu ya Eid Al Adha na Mwenyekiti wa maadhimisho ya sikukuu hiyo jijini Dodoma, Dawood Ismail na kushoto ni Ryadhi Dawood baada ya swala ya Eid katika Uwanja wa Jamhuri Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

HABARI KIMATAIFA

## MAZISHI YA CHILIMA;

# Mjamzito, wengine watatu wafariki msafara wa Makamu wa Rais Malawi

**LILONGWE,** MALAWI

WATU wanne, akiwamo mwanamke mjamzito, wamepoteza maisha baada ya gari lililokuwa kwenye msafara uliokuwa umebeba mwili wa Makamu wa Rais wa Malawi, Saulos Chilima kuwagonga waombolezaji, polisi walisema.

Watu wengine 12 walijeruhiwa katika tukio hilo la jana usiku na walikuwa wakipatiwa matibabu hospitalini.

Ilifuatia mapigano kati ya wenyeji, polisi na wanajeshi waliokuwa wakisindikiza msafara wa marehemu makamu wa rais kutoka mji mkuu, Lilongwe, hadi kijijini kwake kwa mazishi.

Chilima alifariki katika ajali ya ndege wiki moja iliyopita na anatarajiwa kuzikwa leo, wilaya ya nyumbani kwake Ntcheu, kilomita 180 (maili 112) kusini mwa mji mkuu.

Maelfu ya watu walikuwa wamejipanga barabarani, ili kuona jeneza hilo lilipokuwa likisafirishwa kwa mazishi siku ya Jumapili.

Msafara huo ulipopita maeneo ya karibu na nyumbani kwa Chilima, baadhi ya watu walianza kurushia mawe magari ya serikali na viongozi.

Katika ghasia hizo, gari moja lilitoka nje ya barabara na kugonga makundi ya waombolezaji na kuwaua wanne kati yao, kwa mujibu wa taarifa ya polisi.

Msemaji wa Chama cha UTM cha Chilima, aliliambia shirika la habari la AFP kuwa kulikuwa na hali ya wasiwasi njiani, huku waombolezaji wakitaka msafara huo usimame, ili waweze kuona jeneza.

"Huko Dedza, watu walifunga barabara na kutaka kuona jeneza," Felix Njawala alinukuliwa akisema.

Msafara uliendelea baada ya waombolezaji kutulia.

***BBC***



Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, akizungumza na waandishi wa habari jana nchini humo. **PICHA: SABC NEWS**

# Zuma akubali kuungana na Ramaphosa

**JOHANNESBURG,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, amesema chama chake kitaungana na muungano wa upinzani kushirikiana kuipinga serikali.

Hata hivyo anashikilia msimamo wake wa kupinga matokeo ya uchaguzi wa bunge mahakamani.

Chama chake cha uMkhonto we-Sizwe (MK) kitaungana na kile cha Economic Freedom Fighters (EFF), kinachoongozwa na mwanasiasa machachari Julius Malema kilichoshinda viti 39 bungeni katika bunge jipya la Afrika Kusini.

Msemaji wa MK, Nhla-mulo N-dhle-la, amedai licha ya matokeo ya uchaguzi huo kuchakachuliwa, vyama ambayo vitaunda muungano huo wa upinzani vilifanikiwa kupata asilimia 30 katika uchaguzi wa bunge.

Msemaji huyo, alisema matokeo hayo yanawaweka katika nafasi nzuri ya kupigania ukombozi kamili wa kiuchumi wa watu weusi.

Siku ya Ijumaa, MK ilisusia kikao cha kwanza cha bunge huku mpinzani mkuu wa Zuma, Cyril Ramaphosa akichaguliwa kuwa rais wa taifa hilo kwa muhula wa pili.

***DW***

**Msemaji wa MK, Nhla-mulo N-dhle-la, amedai licha ya matokeo ya uchaguzi huo kuchakachuliwa, vyama ambayo vitaunda muungano huo wa upinzani vilifanikiwa kupata asilimia 30 katika uchaguzi wa bunge.**

# Netanyahu avunja Baraza maalum la Mawaziri

**JERUSALEM,** ISRAEL

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amevunja baraza lake lenye mawaziri sita maalumu kwa vita.

Ni wiki moja tu baada ya kuondoka kwa kiongozi wa upinzani, Benny Gantz na mshirika wake Gadi Eisenkot.

Vyombo vya habari vya Israel, viliripoti kuwa masuala nyeti kuhusu vita na Hamas huko Gaza sasa yatajadiliwa na jukwaa dogo.

Netanyahu alikabiliwa na matakwa kutoka kwa mawaziri wa siasa kali za mrengo wa kulia katika muungano wake tawala kujiunga na baraza la mawaziri la vita, ambalo lingeweza kuzorotesha zaidi uhusiano na Marekani na washirika wengine wa kimataifa.

Msemaji wa Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF), alisema kuwa haitaathiri utaratibu wa kiitifaki.

Gantz na Eisenkot walijiuzulu kutokana na uongozi wa waziri mkuu, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mpango wa baada ya vita Gaza.

Wakuu hao wawili wa zamani wa kijeshi, walikuwa wamejiunga na serikali ya umoja wa kitaifa na muungano wa mrengo wa kulia wa Netanyahu siku baada ya kuanza kwa vita Oktoba, mwaka jana.

„Baraza la Mawaziri la vita lilikuwa katika makubaliano ya muungano na Gantz kwa ombi lake.

Mara tu Gantz alipoondoka, hakuna haja ya baraza la mawaziri tena," Netanyahu aliwaambia mawaziri Jumapili, kulingana na Jerusalem Post.

Haaretz iliripoti kwamba baadhi ya masuala yaliyojadiliwa hapo awali na baraza la mawaziri la vita yatahamishwa kwa ajili ya kujadiliwa katika baraza la mawaziri la usalama, ambalo linajumuisha Mawaziri wa Usalama wa Kitaifa na Fedha wa mrengo mkali wa kulia, Itamar Ben-Gvir na Bezalel Smotrich. Ilisema uamuzi nyeti utashughulikiwa katika jukwaa dogo la mashauriano, ambalo lilitarajiwa kujumuisha Waziri wa Ulinzi Yoav Gallant, Waziri wa Masuala ya Mikakati Ron Dermer na Mwenyekiti wa Chama cha Ultra-Orthodox Shas, Aryeh Deri, ambaye alikuwa mwangalizi katika baraza la mawaziri la vita.

Msemaji Mkuu wa IDF, Daniel Hagari alisema Jumatatu kwamba hatua hiyo haitaleta athari.

"Wajumbe wa Baraza la Mawaziri wanabadilishwa na mbinu inabadilishwa. Tuna echelon, tunajua safu ya amri. Tunafanya kazi kulingana na mlolongo wa amri. Hii ni demokrasia," aliwaambia waandishi wa habari.

Jeshi la Israel, lilianzisha kampeni huko Gaza kuiangamiza Hamas kujibu shambulio ambalo halijawahi kushuhudiwa kusini mwa Israel tarehe 7 Oktoba, mwaka jana. Takribani watu 1,200 waliuawa na wengine 251 walichukuliwa mateka.

Zaidi ya watu 37,330 wameuawa huko Gaza tangu wakati huo, kulingana na Wizara ya Afya ya eneo hilo inayoendeshwa na Hamas.

***BBC***

**Wachezaji wa Sayari Womens FC ya Dar es Salaam, wakishangilia baada ya timu yao kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi Daraja la Kwanza Wanawake kwa kuitoa Mount Hanang Queens ya Manyara kwa penalti 5-4. PICHA:TFF**




# Atupakye, Sungura wang'ara uchaguzi soka la wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

ATUPAKYE Jabiri amechaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Chama cha Mpira wa Miguu Wanawake Mkoa wa Mbeya (MWRFA), baada ya kuibuka kidedea katika uchaguzi uliofanyika juzi jijini Mbeya.

Nafasi ya ujumbe wa Mkutano Mkuu wa TWFA ilichukuliwa na Elisia Mwaipopo aliyemwangusha Lina Sanga ambaye alikuwa anashikilia nafasi hiyo.

Asumini Mbuna na Loveness Mwakanyamale walichaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya chama hicho.

Wakati huo huo, Ndinagwe Sungura amepita bila kupingwa katika nafasi ya uenyekiti wa Chama cha Mpira wa Miguu Wanawake cha Mkoa wa Rukwa huku nafasi ya Makamu Mwenyekiti ikienda kwa Jestina Zacharia.

Sharifa Mangosongo alichaguliwa kuwa Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TWFA na Jenisia Mwiga na Cecilia Mapunda wakichaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

Tayari mikoa 18 ya Tanzania Bara imefanya uchaguzi kwa ajili ya kuelekea uchaguzi wa TWFA ambao utafanyika baadaye mwaka huu.

# CHIPUKIZI KUIWAKILISHA Z'BAR KOMBE LA SHIRIKISHO AFRIKA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

RASMI sasa timu ya Chipukizi FC, ndio itakayoiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, imeelezwa.

Chipukizi FC ambayo makazi yake ni Kisiwani Pemba, imepata nafasi hiyo baada ya maamuzi yaliyotolewa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), kupitia kamati yake ya mashindano kuipa ushindi wa 'mezani' timu hiyo.

**Ikumbukwe kwenye mchezo wa fainali wa michuano ya Kombe la ZFF maarufu FA Cup, uliochezwa Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba kwa kuikutanisha timu hiyo dhidi ya bingwa mtetezi wa michuano hiyo, JKU SC, ulishindwa kumalizika baada ya wachezaji wa JKU kumzonga mwamuzi wa kati kwa madai kuwa alikataa bao lao la pili katika dakika za mwishoni za ziada (extra time) baada ya dakika 90 kukamilika timu hizo kutoshana nguvu kwa kufungana bao 1-1.**

Mwamuzi wa mechi hiyo, Mohmed Amour, aliamua kuvunja mchezo huo licha ya kwamba walinda usalama uwanjani hapo walikuwa tayari wameshatuliza vurugu hizo na hali kuwa shwari kwa mchezo kuweza kuendelea.




Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ZFF na kutiwa saini na Ofisa Habari wake, Mohmed Kabwanga, ilieleza kuwa timu ya JKU pia imetozwa faini ya shilingi milioni mbili na kupoteza mchezo huo kwa kosa la wachezaji wake na viongozi wa benchi la ufundi kumfanyia fujo mwamuzi huyo.

Lakini timu ya Chipukizi nayo pamoja na kupewa ushindi, imetozwa faini ya shilingi milioni moja kwa kosa la mashabiki wa timu hiyo kurusha chupa za maji na makopo uwanjani.

Kadhalika mwamuzi wa kati, Amour, naye ameshushiwa rungu la adhabu kwa kufungiwa kuchezesha kwa muda wa miezi mitatu na kutozwa faini ya Sh. 500,000.

Adhabu hizo zote zimetolewa kwa mujibu wa kanuni ya kuendesha mashindano ya ZFF kwa msimu wa 2023/204.

## RUANGWA QUEENS, SAYARI ZAPETA WFDL

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

TIMU ya Ruangwa Queens kutoka Lindi imekuwa ya kwanza kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi Daraja la Kwanza Wanawake baada ya kuifunga Bilo Queens ya Mwanza kwa penalti 4-2 katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Fountain Gate jijini hapa jana.

Timu hizo zililazimika kwenda hatua ya matuta baada ya kutoka sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida, Christer Basil akifunga kwa upande wa Ruangwa na Pili Tandika aliisawazishia Bilo Queens.

Katika mechi nyingine iliyochezwa jana asubuhi Sayari Womens ya Dar es Salaam iliifunga Mount Hanang Queens ya Manyara kwa penalti 5-4 baada ya kumaliza dakika 90 za kawaida kwa sare ya bila kufungana.

Mechi nyingine za hatua ya robo fainali zilizotarajiwa kufanyika jana jioni ilikuwa ni kati ya Gets Program ya Dodoma dhidi ya Mwanga City Queens kutoka Kigoma huku Mlandizi Queens ya Pwani ikipambana na Mkwawa Queens kutoka mkoani Iringa.

Timu mbili zitakazotinga hatua ya fainali katika ligi hiyo itakayomaliza mwishoni mwa wiki zitapanda daraja moja kwa moja kucheza Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), msimu ujao wa 2024/2025.

## ZISIKUPITE

### SIMONS AGOMBEWA

KLABU za Manchester United, Arsenal, Manchester City na Bayern Munich, zote zimeonesha nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Uholanzi na Paris St-Germain, Xavi Simons mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### LIVER YAKATALIWA YORO

OFA ya Liverpool ya euro milioni 50 kumnunua mlinzi wa Lille, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18. imekataliwa. ***(Mundo Deportivo)***

### COLWILL HAKAMATIKI

JITIHADA za Bayern Munich kumnasa mlinzi wa Chelsea na England, Levi Colwill mwenye umri wa miaka 21, zimegonga mwamba, huku timu hiyo ya Ujerumani ikizingatia ada yoyote ya uhamisho kwa nyota huyo kuwa juu sana. ***(Sky Sports Ujerumani)***

### IHEANACHO AFUATILIWA

KLABU ya Aston Villa inamfuatilia mshambuliaji wa Leicester City, Kelechi Iheanacho mwenye umri wa miaka 27, anapojiandaa kuondoka msimu huu wa majira ya joto kwa uhamisho wa bila malipo. ***(Football Insider)***

### MAATSE ANYATIWA

ASTON Villa pia inawasiliana kila siku na Chelsea kuhusu kutaka kumnunua beki wao wa pembeni, Ian Maatse mwenye umri wa miaka 22, ambaye yuko kwenye kikosi cha Uholanzi cha Euro 2024. ***(Football Insider)***

### CANCELO BEI JUU

MANCHESTER City hawatakubali dau la chini ya pauni milioni 25 kwa mlinzi wa Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 30, huku Barcelona wakiwa na nia ya kumsaini kwa mkataba wa kudumu baada ya muda wa mkopo. ***(Sun)***

### GREAVES KUMRITHI BRANTHWAITE

KLABU ya Everton inamtazama mlinzi wa Hull City, Jacob Greaves mwenye umri wa miaka 23, kama anayeweza kuziba nafasi ya beki wao wa kati, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, ikiwa ataondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(Hull Daily Mail)***

### DAVIES, BAYERN BADO

KLABU ya Bayern Munich haijafanikiwa kukubaliana mkataba mpya na beki wa kushoto wa Canada, Alphonso Davies, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid, lakini hawana mpango wa kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 na kumruhusu kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake nao. ***(Sky Sports Ujerumani)***

### RODIN AGOMBEWA

KLABU za Ipswich, Southampton, Leicester na Leeds United ni miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili mlinzi wa Wales na Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 26, Joe Rodon. ***(Soka.London)***

### MATS AWANIWA ROMA

AS Roma inalenga kumnunua beki wa Ujerumani, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, ambaye kuondoka kwake Borussia Dortmund kumethibitishwa. ***(Calciomercato)***

## DOND… ZA …OKA MAGA… …A



# BELLINGHAM AMEANDIKA HISTORIA YAKE - SOUTHGATE

**Ni baada ya kuipa ushindi England kwenye Euro 2024, asema ni wakati wa...**

**GELSENKIRCHEN,** UJERUMANI

GARETH Southgate amesema Jude Bellingham „ameandika historia yake" baada ya kiungo huyo wa Real Madrid kuwapa ushindi England katika mechi yao ya kwanza ya Kundi C kwenye Euro 2024 dhidi ya Serbia Jumapili.

Bao la kichwa la Bellingham dakika ya 13 lilitosha kuwapa "Simba Watatu" hao ushindi wa 1-0 mjini Gelsenkirchen huku onesho la kuvutia la kipindi cha kwanza likisababisha kipindi cha pili kuwa na mvutano.

Hata hivyo, Bellingham alikuwa mchezaji bora wa England - akitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mechi na Southgate alisema: "Anaandika wasifu wake mwenyewe.

"Wakati wa kukimbia kwake. Ilikuwa mchezo mzuri sana katika kutayarisha goli pia. Nilifikiri kwa nyakati tofauti, wachezaji wetu wote wa mbele walionekana hatari na walifanya kazi nzuri kwa timu."

England waligonga mwamba wa goli katika kipindi cha pili kwa mpira wa kichwa wa Harry Kane dakika ya 77, huku golikipa wa Serbia, Predrag Rajkovic, akifanya kazi ya ziada.

"Timu hii bado inakuja pamoja," alisema Southgate.

„Kila mtu anatarajia tufanikiwe, lakini kuna kazi ngumu sana mbeleni. Tuna upungufu wa mambo fulani. Tunatafuta suluhu bora zaidi.

"Tumekuwa na mchujo mgumu sana kwa haya yote kutokana na majeraha, lakini ari ya kundi ilikuwa pale kwa kila mtu kuona usiku wa leo na bila shaka tutakuwa kutokana na hilo."

Kwa upande wa Bellingham, alisema fomula ya mafanikio yake ilikuwa juu ya kila mtu mwingine katika maisha yake, akiondoa uangalizi baada ya kuikokota England kwa ushindi muhimu wa ufunguzi wa mashindano hayo.

# MBAPPE HATACHEZA OLIMPIKI

**MUNICH,** UJERUMANI

KYLIAN Mbappe amethibitisha Jumapili kuwa hataichezea timu ya Olimpiki ya Ufaransa kwenye Michezo ya Paris kwani klabu yake mpya ya Real Madrid inapingana na wazo hilo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alisema mnamo Machi kwamba alikuwa na nia ya kucheza kwenye michezo yake ya nyumbani, lakini kwa kuwa mashindano ya mpira wa miguu ya Olimpiki hayapo kwenye Kalenda ya FIFA klabu hazilazimiki kuwaachia wachezaji wao.

Mbappe hakujumuishwa katika kikosi cha wachezaji 25 cha awali kwa ajili ya Olimpiki mapema mwezi huu, ingawa Kocha Mkuu, Thierry Henry, aliacha mlango wazi.

"Msimamo wa klabu yangu ulikuwa wazi sana, kwa hivyo kuanzia wakati huo, nadhani nilijua sitashiriki," alisema Mbappe akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mechi ya jana ya Kundi D dhidi ya Austria kwenye Euro 2024.

"Hivyo ndivyo ilivyo, na ninaelewa hilo pia. Ninajiunga na timu mpya Septemba, kwa hivyo si njia bora ya kuanza safari.

"Nitaitakia timu hii ya Ufaransa kila la heri. Nitatazama kila mchezo. Natumaini watashinda medali ya dhahabu."

Mashindano ya soka ya wanaume ya Olimpiki yanaanza Julai 24, siku 10 baada ya fainali ya mashindano ya Euro kumalizika.

## Weghorst akasirika kuanzia benchi Uholanzi

**HAMBURG,** UJERUMANI

KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman, amesema Wout Weghorst „amekasirishwa" kwa kuambiwa kwamba anaweza kuanzia benchi katika Euro 2024 baada ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester United kufunga bao la ushindi dakika za lala salama katika ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Poland dakika chache baada ya kuingia kwenye mchezo kama mchezaji wa akiba.

Weghorst mwenye umri wa miaka 31, alichukua nafasi ya Memphis Depay katika dakika ya 82 ya mechi ya Kundi D mjini Hamburg na akafunga muda mfupi baadaye kwa pasi ya Nathan Ake.

Waholanzi hao walikuwa wamekosa nafasi nyingi za wazi dhidi ya Poland ambao bao lao la kwanza la Adam Buksa lilisawazishwa na Cody Gakpo, kabla ya Koeman kumwingiza Weghorst.

Baada ya mshambuliaji huyo kufunga bao lake la saba katika mechi 11 za kimataifa na kuifanya timu yake ipate ushindi, Koeman alisema amelazimika kumwambia Weghorst kwa nini anaamini ana hatari zaidi kwenye michezo akitokea benchi.

"Nilipozungumza na Wout mwanzoni kuingia timu ya taifa, nilijaribu kueleza kila mchezaji mmoja mmoja uwezekano wa kuanza au kuingia uwanjani katika kipindi cha pili tunapohitaji mchezo tofauti," alisema Koeman.

"Alikasirika kidogo, na nadhani hiyo ni majibu mazuri. Wout amekasirika na anafanya mengi kupata nafasi ya kuanza. Hayo ni mawazo mazuri kutoka kwa mchezaji na mara zote uamuzi wa mwisho wa kocha.

"Bao lake lilishangiliwa na umati wa watu ambao ni dhahiri kwa sababu alizifumania nyavu ambazo zilikuwa na uamuzi kwa wakati huu, ana thamani kwa timu, ana tabia tofauti ambayo ni kubwa na tuliyohitaji.

"Ilipaswa kuwa 4-1 kwetu baada ya saa moja, lakini hatukuweza kuzifumania nyavu, ilikuwa hatari kwetu kwa sababu kikosi cha Poland kilikaribia kupata goli lakini tulikuwa na bahati na kufunga bao la pili. „

Weghorst, ambaye sasa anakipiga nchini Ujerumani katika klabu ya Hoffenheim, amekuwa na tabia ya kufunga mabao muhimu akitokea benchi.

"Leo ni kama vile unavyotumaini au kufikiria mapema. Kuwa na uwezo wa kuwa muhimu tena kwa njia hii ni nzuri sana," alisema Weghorst akiiambia ESPN Uholanzi baada ya mchezo."




## Mkataba mpya wa Man United bado - Ten Hag

**MANCHESTER,** ENGLAND

ERIK ten Hag amesema bado hajakubali mkataba mpya na Manchester United na alikiri kwamba "haitafanyika kirahisi" baada ya kuambiwa na utawala mpya wa klabu hiyo kwamba kibarua chake kiko salama katika timu hiyo ya Ligi Kuu England.

Ten Hag aliarifiwa na bodi ya soka inayoongozwa na Ineos wiki iliyopita kwamba hatafutwa kazi kama kocha baada ya kushinda Kombe la FA, licha ya timu hiyo kumaliza katika nafasi ya nane kwenye ligi.

Lakini baada ya kukubali kubaki na kocha huyo wa zamani wa Ajax, vyanzo viliiambia ESPN kwamba Ineos iko tayari kuongeza mkataba wa Ten Hag zaidi ya miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake uliopo.

Ten Hag sasa amesema mazungumzo zaidi yanahitajika na United, ambao walimthibitishia kwamba walizungumza na kocha wa zamani wa Bayern Munich, Chelsea na Paris Saint-Germain, Thomas Tuchel, kuhusu kuchukua nafasi yake.

"Manchester United na mimi bado tunapaswa kutafuta makubaliano ya mkataba mpya," alisema Ten Hag akilimbia Shirika la Utangazaji la Uholanzi, NOS.

„Hii haifanyiki kwa urahisi, bado tutalazimika kuzungumza juu ya hili.

"United wameniambia kwamba walizungumza na Tuchel, lakini hatimaye walifikia hitimisho kwamba tayari wana kocha bora."

Ten Hag, ambaye alijiunga na United mwaka 2022, alisema alikutana na maofisa wa klabu likizoni kwenye kisiwa cha Ibiza nchini Hispania ili kutatua mustakabali wake.

"Manchester United walisumbua likizo yangu, ghafla walisimama mlangoni kwangu," alisema. „Walikuja kwangu huko Ibiza."

HABARI MICHEZO

# BINGWA LIGI KUU ZANZIBAR SASA KUJULIKANA IJUMAA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Kuu ya Zanzibar msimu wa 2023/24 inatarajia kufika tamati Ijumaa wiki hii na kumpata bingwa atakayeiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Ligi ya Mabigwa Afrika.

Ligi hiyo ambayo kwa sasa ipo katika mzunguko wa 29 imebakiza mzunguko mmoja ili kukamilika kwa msimu.

Hata hivyo, bado ni vigumu kutabiri timu itakayoweza kutwaa ubingwa huo kutokana na timu mbili za juu katika msimamo, JKU na Maafande wa Zimamoto, kila moja kuwa katika nafasi nzuri ya kulibeba taji hilo.

JKU ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 62 ikifuatiwa na Maafande wa Zimamoto wenye alama 61, hivyo mechi za mwisho ndizo zitakazoamua timu itakayotwaa ubingwa msimu huu.

Mabingwa watetezi wa ligi hiyo, KMKM SC, tayari wameshapoteza nafasi ya kutetea taji hilo kutokana na kushika nafasi ya tatu kwenye msimamo kwa kujikusanyia pointi 54 hadi sasa.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka la Zanzibar (ZFF), mzunguko wa 29 wa ligi hiyo utaendelea leo kwa kupigwa michezo ambayo huenda ikaamua Bingwa wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

Vinara JKU watashuka uwanjani kuvaana na KMKM katika Uwanja wa Amaan B wakati Zimamoto wenyewe watavaana na wakongwe Mlandege FC katika dimba la Mau A.

Kwa upande wa timu ambazo zinapambana kubaki Ligi Kuu, utapigwa mchezo mmoja ambapo Malindi SC watavaana na New City FC katika Uwanja wa Mau B.

Katika mechi za mzunguko wa 29 zilizopigwa juzi timu ya Mafunzo ilitoshana nguvu na Kipanga FC kwa kufungana mabao 3-3 mchezo uliopigwa Uwanja wa Mau A, wakati Kisiwani Pemba katika Uwanja wa FInya, Jamhuri SC na Chipukizi FC nazo zilitoka sare ya bao 1-1.

EURO 2024...



Mshambuliaji wa Denmark, Rasmus Højlund, akijaribu kufunga lakini kipa wa Slovenia, Jan Oblak, akiwa makini kumzuia kwenye mechi ya michuano ya Euro iliyopigwa Ujerumani juzi na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga yageukia ngumi

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umeahidi kutia mkono pambano la ‚Dar Boxing Derby' litakalofanyika Juni 29, mwaka huu katika viwanja vya Posta vilivyopo Kijitonyama, Dar es Salaam, kwa kuwa miongoni mwa wadhamini.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ally Kamwe, alisema mchezo wa ngumi kwa sasa unapiga hatua kutokana na mabondia wa Tanzania kufanya vizuri katika mapambano yao.

Alisema ‚Dar Boxing Derby' ni pambano lililojaa ubunifu mkubwa kwani mabondia ambao watacheza siku hiyo ni wale wenye viwango vikubwa.

„Yanga tumethibitisha tutadhamini pambano hilo kwa sababu tunajua kuna vipaji vingi vitaonekana siku hiyo, pia tutachagua mabondia ambao wana mapenzi na klabu yetu tutawasajili kwa lengo la kufufua ngumi kwenye klabu yetu," alisema Kamwe.

Kamwe alisema kama klabu watatoa zawadi kwa mabondia ambao watafanya vizuri, ikiwamo pambano kuu kati ya Nassib Ramadhan na Juma Choki.

Naye, promota wa pambano hilo, Meja Selemani Semunyu, ameziomba klabu nyingine ziwekeze katika ngumi kwa sababu mchezo huo una vijana wengi wenye vipaji. „Ni faraja kuona klabu kubwa kama Yanga imekubali kudhamini ngumi kwa sababu wameona vipaji mbalimbali ambavyo vinatoka katika mchezo huu, milango ipo wazi kwa klabu zingine kuja kuunga mkono," alisema Semunyu.

Semunyu alisema mbali ya pambano la Nassib Ramadhan na Juma Choki, mabondia wengine watakaopanda ulingoni ni Tonny Rashidi ambaye atacheza na Oscar Richard, wakati Said Bwanga atapigana na Said Mkola, huku Haidari Mchanjo akitoana jasho na Charles Tondo, wakati pia akina dada Najma Isike akivaana na Nasra Msami.

## Simba yafuata beki kisiki Asec

INATOKA UK. 24

fasi ya Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu, ambapo pia alikuwa mjumbe wa bodi upande wa mwekezaji.

Mo pia aliipongeza timu ya Simba Queens kwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara kwa upande wanawake, akiahidi kukuta nao kabla ya msimu kuanza na kuwapa zawadi.

"Nichukue nafasi hii kuipongeza timu yetu ya Simba Queens, kwa kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara, muda si mrefu nitapata muda wa kukutana nao kabla ya msimu kuanza, nitawapa zawadi yangu binafsi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kupeperusha bendera ya Simba, hongereni sana Simba Queens," alisema.

Aliwapongeza pia vijana wa Simba chini ya miaka 20 kwa kufikia hatua ya nusu fainali ya ligi hiyo, na chini ya miaka 17 ambayo inafanya vema katika ligi ya vijana wa umri huo.

Wakati hayo yakiendelea, klabu hiyo inadaiwa kuanzisha mazungumzo na beki wa kati Asec Mimosas, Tra Bi Tra ili kuziba nafasi ya Inonga.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinaeleza kuwa mazungumzo yameanza ingawa bado hayajafika mwisho.

"Tuna tatizo la beki mkakamavu. Tangu alipoondoka Joash Onyango tumeonekana kuyumba sana, Fondoh Che Malone na Inonga wanaonekana wana aina moja ya uchezaji na hawatumii nguvu, na siyo wagonganaji, hivyo mastraika hawaogopi, huyu anayefuatiliwa yupo vizuri kote kote, ana akili ya mpira na mpambanaji," alisema mtoa taarifa.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinaeleza kuwa tayari dili la Inonga kwenda FAR Rabat limekamilika, ambapo kuna makubaliano yamefanyika baina ya pande zote tatu na huenda akatua kwa klabu yake hiyo mpya hivi karibuni.

Wakati huo huo Klabu ya Simba imetangaza rasmi nahodha wao, John Bocco, hatakuwa sehemu ya kikosi chao msimu ujao, lakini pia ikiweka wazi kuwa imempa majukumu mapya ya kuwa kocha wa timu ya vijana ya chini ya umri wa miaka 17.

## Yanga kuileta Mamelodi

INATOKA UK. 24

Yanga pia inatajwa kuwa mbioni kumsajili winga wa timu hiyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Emmanuel Bola Lobota, aliyekuwa kwenye kiwango cha juu msimu huu, hasa baada ya kumkosa Philippe Kinzumbi wa TP Mazembe ambaye ameikacha timu hiyo na kutimkia, Raja Casablanca ya Morocco.

Wengine wanaotajwa kuwa huenda wanaweza kuvaa uzi wa kijani na njano ni kiungo mshambuliaji, Charve Onoya na kiungo mkabaji, Agee Basiala, wote wanakipiga katika Klabu ya AS Maniema Union na beki wa kushoto, Chadrack Boka kutoka Klabu ya Saint Eloi Lupopo, wote kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Michezo
Nipashe
Jumanne Juni 18, 2024

## Bellingham ameandika historia yake - Southgate



UKURASA 21

# SIMBA YAFUATA BEKI KISIKI ASEC

## ●●●Mo naye aingiza sura tatu mpya huku klabu ikiagana rasmi na Bocco...

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

WAKATI Mwekezaji, Rais wa Heshima na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji, akitangaza wajumbe sita upande wake, zikiwamo sura tatu mpya, klabu hiyo imetajwa kuanzisha mazungumzo na beki wa kati wa Asec Mimosas ya Ivory Coast, Anthony Tra Bi Tra ili kuziba nafasi ya Henock Inonga ambaye taarifa zinaeleza ameshamalizana na FAR Rabat ya Morocco.

Akizungumza juzi usiku, Mo, pamoja na mambo mengine, aliwatangaza wajumbe sita upande wa mwekezaji kuziba nafasi za wale waliojiuzulu hivi karibuni, watatu wakiwa wapya akiwamo mjumbe wa zamani wa bodi hiyo na Ofisa Mtendaji Mkuu, Crescentius Magori.

Wengine ni Mohamed Nassor na Hussein Kita, huku watatu pia wakirejeshwa ambao ni Salim Abdallah 'Try Again' ambaye alimtangaza siku chache zilizopita, Mbunge wa Jimbo la Mlalo, Rashid Shangazi na Zulfikar Chandoo.

Sura mbili ambazo hazipo katika bodi hiyo ni Dk. Rafael Chegeni na Hamza Johari, ambao kwa mujibu wa Mo wameomba wasijumuishwe kutokana na kutingwa na majukumu mengine.

"Johari, ameomba apumzike kwa ajili ya majukumu ya kikazi, lakini nimemuomba aingie kwenye Baraza la Ushauri, na Rafael Chegeni, ameomba apumzike kwenye Bodi ya Simba, maana ana bodi nyingi anazohudumu kwa sasa, ila ataendelea kuwa mshauri na mtu muhimu sana katika familia ya Simba," alisema Mo, wakati wa kutangaza wajumbe hao.

Kabla ya kurejeshwa ujumbe wa bodi, Magori alikuwa ni Mshauri Binafsi wa Mo kwenye masuala ya michezo, na kabla ya hapo aliwahi kuhudumu na-

INAENDELEA UK. 23

**SUBIRI...**



Mshambuliaji wa England, Harry Kane, akipunguzwa kasi kwa kuvutwa bega na kiungo wa Serbia Sergej Milinkovic-Savic, kwenye mechi ya michuano ya Euro iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Veltins-Arena, Ujerumani. England ilishinda bao 1-0. Habari UK 21. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga kuileta Mamelodi Siku ya Mwananchi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imetajwa kukamilisha usajili wa golikipa wa Ihefu FC, ambayo kwa sasa imebadili jina na kuitwa Singida Black Stars, Khomein Abubakar, kuchukua nafasi ya Metacha Mnata huku pia ikitangaza kuileta Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, Wiki ya Mwananchi Agosti, mwaka huu.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema kuwa kama mambo yatakwenda yalivyopangwa basi safari hii Yanga itakipiga dhidi ya timu hiyo ambayo ilicheza nayo katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika michezo miwili Dar es Salaam na Afrika Kusini, timu zote zikishindwa kufungana kabla ya wawakilishi hao wa Tanzania kuondolewa kwa mikwaju ya penalti 3-2.

"Kama alivyosema siku chache nyuma Rais wa Klabu, Injinia Hersi kuwa tuna mwaliko Kenya kwa ajili ya kwenda kufungua uwanja na Afrika Kusini ambako tumealikwa na Mamelodi Sundowns, sasa na sisi pia tumeamua kuwaalika kwenye kilele cha Wiki ya Mwananchi kuelekea msimu ujao wa mashindano, kama mambo yataenda kama yalivyopangwa tutakipiga nao siku hiyo," alisema Kamwe.

Wakati hayo yakiendelea, chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo kinasema klabu hiyo imemsajili, Khomein baada ya mapendekezo ya benchi la ufundi chini ya Miguel Gamondi, akiwa ni mchezaji wa kwanza Mtanzania kusajiliwa na Yanga msimu huu.

„Ilikuwa ni lazima kwanza tupate kipa mzawa ili awe mbadala wa Diarra, na kulikuwa na machaguo kadhaa ambayo tumeyakosa, hatimaye tumeangukia kwa Khomein, ila ni mmoja wa makipa wazuri sana, alionyesha kiwango kikubwa msimu huu akiwa na kikosi cha Ihefu, mpaka benchi la ufundi likatoa pendekezo la kusajiliwa," kilisema chanzo hicho.

Taarifa zinasema awali, Yanga ilikuwa ikimhitaji kwa udi na uvumba golikipa wa Prisons, Yona Amosi, ikashindikana, baadaye ikahamia kwa kipa wa Geita Gold, Costantine Malimi na mwishoni ikaangukiwa kwa Khomein.

Kabla ya kujiunga na Ihefu, Khomein alikuwa kipa wa Geita Gold ambako alifanya vema akiwa langoni.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >